

MASWALI NA MAJIBU JUU YA

KITABU CHA MWANZO

 Sasa, kama ye yote ana swali lo lote wanalotaka kulileta, basi, hebu yasogezeni tu juu hapa, acha mtoto fulani ayaleta au vyo vyote mtakavyo. Au, labda, tukimaliza... Ni—ninayo sita hapa kwa ukurasa mmoja, na ndipo hapa, ndipo tunayo mawili pale.

² Sasa, tu—tunataka kuchunguza. Sababu ya kufanya haya ni kutambua nini kilicho kwenye mawazo ya watu, yale wanayowaza. Ona? Na hilo ndilo lifanyalo kanisa nzuri na imara. Yakubidi kuwa na—na nyakati, kama tu vile uendavyo kuondoa kwekwe, mwajua, na kuondoa kila kitu njiani ili uweze kusogea mbele kwa uthabiti. Kwa hivyo sasa hiyo ndiyo sababu tuna usiku wa maswali mara kwa mara, ni kuchunguza.

³ Sasa, kama kuna swali lo lote ambalo... Sasa, wakati huu niliyafungua, wazi sana. Nami nilisema... Sasa, ningesema, “Sasa, kama ye yote... kitu cho chote tu kina—kinachohusu Maandiko; jibu. Uliza.” (Asante, ndugu.) Na nilisema, “Cho chote kinachohusika na Maandiko; jibu.” Ona, nasi tungekijibu. Lakini usiku huu nilisema...

⁴ Mwajua, ndipo wanakuja, wanasema, “Ndugu Bill,” wakanikuliza mimi swali, “je, wadhani kama—kama—kama Si *Fulani* alifanya *jambo fulani*, je, huo ni Ukristo?”

⁵ Vema, hilo ni kama kumwingilia mtu fulani. Lakini nilisema, “Hebu wawe na hayo usiku huu.” Ona, hayo ni sawa. Ili tuweze tu kupata kama kuna mvutano wo wote.

⁶ Ee ni—ni—ninajisikia vizuri sana usiku huu. Nilikata nyasi adhuhuri yote, kwa hivyo najisikia vizuri sana, nje kwenye jua kali.

⁷ Tuna m—mkutano unaokuja hivi karibuni sasa, msisahau. Agosti ishirini na tatu, kwenye uwanja wa michezo Chicago, hadi September tano. Tarajieni wakati furaha katika Bwana kule. Na imetangazwa kote sasa, na magazeti mbali mbali yanautangaza. Nasi tunatarajia wakati wa furaha.

⁸ Sasa, ninayo moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, nadhani, katika ukurasa mmoja hapa. Na karibu yote yanahusu jambo lile lile, nyuma katika—katika Kitabu cha Mwanzo.

⁹ Sasa, kwanza ni Mwanzo 1:26, au 1:26 hadi 28, ndipo ambapo yu—yule mtu na... waliuliza ingekuwaje. Vipi—vipi swali hili... nakusudia, aliuliza swali, kunradhi. Nasi tunataka kusoma hilo kwanza. Sasa, waliliandika hapa. Mkitaka

kulifuatilia toka nyuma, ni vema. Kasema, “Mungu akaumba mtu, mwanamume na mwanamke aliwaumba.” Ona? Na ndipo linalofuata yeye amepata Mwanzo . . . au mwanaume au mwanamke, mmojawao, ameandika Mwanzo 2:7, “Akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi.” Hapo ni mahali pengine. Nitapasoma pote, ili tuyapate yote pamoja ili mweze kuona. Sasa la kwanza, fungu la kwanza la hili ni, sasa lilisema:

1. “Mungu alimuumba mtu, mwanamume na mwanamke. Alimuumba mtu, mwanamume na mwanamke.” Sasa hilo ni, nafikiri, jambo la kwanza. **Sasa katika Mwanzo 2:7, inasema “Akamfanya,”** (limepigwa mstari) **“Lakini kwanza Yeye aliumba.”** Ndipo . . . yeye amepiga mstari chini ya hayo. **“Na akamfanya”** (limetiwa mkazo) **“mtu kwa mavumbi ya ardhi akampulizia puani”, na mengineyo. Sasa, tofauti ni nini, au Maandiko haya yaliyo juu hapa yana uhusiano gani?**

¹⁰ Sasa, hili ni . . . Sasa, kama umeliandika, Mwanzo 1:26 hadi 28, na Mwanzo 2:7. Sasa, ni jambo la harara sana, nami—nami huenda nisi . . . Nina wazo langu binafsi juu yake, kwa hivyo nitawapeni ninyi jinsi nionavyo mimi. Na kama hukubaliani nami, vema, si hoja.

¹¹ Nataka kumpongeza Ndugu Neville kwa yale majibu mazuri aliyotoa kwa maswali yale pale. Sasa, ni mazuri.

¹² Naam, katika hili, Mwanzo 1:26, Mungu alimuumba mtu kwa mfano Wake Mwenyewe. Na kama mngeangalia, tutayapata ili mweze kuyasoma, na 26 . . . Kama mgependa kusoma pamoja nasi, tutawafurahieni—mkifanya vile, nithibitisheni.

“Mungu akasema, Na tufanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatawale samaki wa baharini, . . . na ndege wa angani, . . . na wanyama wa nchi, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi.

Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimuumba, mwanaume na mwanamume na mwanamke aliwaumba.

¹³ Sasa, hilo ni . . . nimelisikia hilo likibishani mara nyingi, na ulimwenguni kote, ubishi huzuka kwa hilo. Sasa katika Mwanzo 2:7 tazama kile Yeye alifanya hapa. Vema, liko hapa:

Na . . . Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, akampulizia puani pumzi ya uhai, mtu akawa nafsi hai.

¹⁴ Sasa, ni kufanywa namna gani . . . Mwuliza swali yu—yule ataka kuuliza:

Kuna uhusiano gani kati ya Mwanzo 1:26 na Mwanzo 2:7? Mungu aliwaumba watu wawili. Na mtu yule alikuwa nani, na nani . . . Hilo lina uhusiano gani? Nini . . . linawianaje na Maandiko?

¹⁵ Vema, basi, kama mtachunguza kwa makini sasa, katika Mwanzo 1:26, hebu tupate kwanzo sehemu ya kwanza. Mungu

alisema, “Na *tu*.” Sasa, “na *tu*,” *tu*- ni... “Na tufanye mtu kwa mfano wetu.” *Wetu*, bila shaka, twatambua Yeye anaongea na mtu fulani, Yeye alikuwa anaongea na kiumbe kingine. “Na tufanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu, akatawale wanyama wa nchi.”

¹⁶ Ukichunguza, katika uumbaji, kitu cha kwanza kilichoumbwa, bila shaka, kilikuwa nuru. Fuatisha moja kwa moja viumbe vyote, kitu cha mwisho kuumbwa kilikuwa nini? Mwanamume. Na mwanamke alifanywa baada ya mwanamume. Vema, cha kwanza... Kitu cha mwisho kilichoumbwa, cha uumbaji wa Mungu, ni mwanadamu.

¹⁷ Lakini Mungu alipomuumba mtu Wake wa kwanza, ukichunguza, Yeye alimfanya kwa sura Yake Binafsi, Yeye aliumbwa kwa mfano wa Mungu. Na Mungu ni nini? Sasa, kama twaweza kutambua Mungu ni nini, tunaweza kutambua Yeye aliumba mtu wa aina gani.

¹⁸ Sasa katika Yohana Mt. sura ya 4, nami nita... tutasoma haya. Yesu akimzungumzia mwanamke yule katika kile... kama mngenda kuifungua. Mimi... kwa kutokuwa na wakati mwingi, singeweza kuyaandika, ilinibidi tu niyashikilie tu mawazoni. Nanyi yatafuteni sasa, kama naweza kuyapata upesi sana. Sasa, hebu tuanzie sura ya 4 hivi, na kifungu cha 14:

Walakini ye yote atakayekunywa maji yale nitakayompa mimi hataona kiu milele;...na yawe chemchemi ya maji, yakibubujikia uzima wa milele.

Yule mwanamke akamwambia, Bwana, unipe maji hayo...nisije hapa kuteka.

Yesu akamwambia...Nenda kamwite mumeo...Yule mwanamke akajibu...

¹⁹ Naamini yatubidi tusome juu ya hapo sasa, kupata, tupate kile—kile ninachowatakeni mkione hapa. Labda sipo, labda naweza kupapata chini hapa, na kile ninachotaka kuona. Wasemaje? Kifungu cha 23 na 24. Vema.

Ninyi mnaabudu... (naam)...Ninyi mnaabudu msichokijua; sisi tunaabudu tukijuacho; kwa kuwa wokovu watoka kwa Wayahudi. (na ndivyo hasa, ona)

Lakini saa inakuja,...Lakini saa inakuja, nayo sasa ipo, ambayo waabuduo halisi (Myahudi au Mtaifa) watamwabudu Baba katika roho na kweli. Kwa maana Baba awatafuta watu kama hao wamwabudu.

²⁰ Sasa kifungu kinachofuata ndicho ninachotaka;

Mungu ni Roho, nao wamwabuduo yeye imewapasa kumwabudu katika roho na kweli.

²¹ Sasa, kama Mungu alimuumba mtu katika mfano Wake Binafsi na katika sura Yake, Yeye alimwumba mtu wa aina

gani? Mtu wa roho. Sasa, ukichunguza, baada ya Yeye kuviumba vitu vyote, na kumuumba mtu wa roho, kusoma haya kwa makini sasa (kwa yule aliyeuliza swali hili) twapata hili, kwamba Mungu alimpa mtu huyo utawala wa wanyama na samaki na kila kitu. Lakini, katika kufanya Kwake pale Yeye alimwumba mtu kwa mfano Wake Mwenyewe kuwaongoza ng'ombe, kuwaongoza wanyama wa makondeni, kama tu vile Roho Mtakatifu amwongozavyo mwamini siku hizi. Ona?

²² Yeye alikuwa, kwa maneno mengine, Adamu, mtu wa kwanza katika viumbe vya chini vya Mungu. Kiumbe cha kwanza kilikuwa Mungu Mwenyewe; ndipo toka kwa Mungu kukaja Logos, ambayo ilikuwa Mwana wa Mungu; ndipo toka kwa Logos, ambayo ilikuwa lile Neno ("Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu, Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu."), toka kwa Logos kukaja mwa—mwanadamu.

²³ Ee nina mfano malidadi mawazoni mwangu sasa, kama mnaweza kushika safari ndogo pamoja nami. Naamini nimeueleza hapo awali, lakini kulifikisha hili mahali ambapo bila shaka mtaliona. Sasa, hebu tushike safari ndogo na kurudi nyuma kwa muda mdogo. Sasa, usiwaze jinsi kulivyo na joto, hebu tuweke mawazo yetu moja kwa moja kwa lile tutakaloongea na kuliwazia sasa.

²⁴ Hebu turudi nyuma miaka milioni mia moja kabla hata nyota, mwezi wala cho chote ulimwenguni hakijakuwepo. Sasa kulikuwa na wakati ambapo hakukuwa na cho chote hapa, ilikuwa tu dawamu na Milele. Na kote kote na Milele ilikuwa Mungu, Yeye alikuwako hapo mwanzo.

²⁵ Naam, hebu tuende nje hapa kingoni mwa ngazi hii na kutazama kule tuone vitu vikitendeka.

²⁶ Basi, "Hakuna mtu aliyemwona Baba wakati wo wote." Hakuna mtu awezaye kumwona Mungu katika jinsi ya mwili, kwa sababu Mungu hayuko katika mwili, Mungu ni Roho. Ona? Vema. "Hakuna mtu aliyemwona Baba, bali Mwana pekee wa Baba ndiye aliyemfunua." Yohana . . . wa kwanza, ona.

²⁷ Sasa, lakini tazama sasa, hakuna cho chote, ni anga tu. Hamna nuru, hamna giza, hamna cho chote, inaonekana kana kwamba hamna cho chote. Lakini ndani mle kuna Kiumbe kikubwa cha kimbinguni, Yehova Mungu, aliyefunika anga la mahali pote wakati wote. Yeye alitoka milele hata milele, Yeye ndiye chanzo cha uumbaji. Huyu ni Mungu. Hakuonekana cho chote, hakisikiki cho chote, hamna atomi iliyosogezwa hewani, wala cho chote kile, hamna hewa, wala cho chote kile, bali Mungu alikuwepo. Huyu alikuwa Mungu. (Sasa, hebu tuchunguze kwa dakika chache, na baada ya muda mchache. . .) Hakuna mtu amemwona Huyu, sasa, Huyu ni Baba. Huyu ni Mungu, aliye Baba.

28 Sasa tazama. Ndipo baada ya kitambo kidogo naanza kuona Nuru ndogo takatifu ikianza kuumbika, kama duara ya mwanga au kinginecho, ungeiona tu kwa macho ya kiroho.

29 Lakini tazama sasa, hali tunapotazama, kanisa lote sasa. Tunasimama katika ngazi kubwa mno, tukitazama anayotenda Mungu. Na tutafikia swali hili hapa nanyi mtaona jinsi anavyoliingiza.

30 Sasa, hakuna mtu aliyemwona Mungu. Na sasa, jambo tunaloanza kuona, kwa macho ya kutazamia rohoni, twaona Nuru ndogo nyeupe ikiumbika nje pale. Hiyo ni nini? Hiyo iliitwa, na wasoma-Bibilia, “Logos,” au “mtiwa mafuta,” au “upako,” au ile...kama nilivyotaka kusema, se—sehemu ya Mungu ikaanza kuumbika kuwa kitu fulani ili wanadamu wapate kujua jinsi ilivyokuwa. Ilikuwa kidogo, chini...au Nuru ndogo, ikisongea. Yeye...Hiyo ilikuwa Neno la Mungu.

31 Sasa Mungu alijizalia Mwana huyu ambaye aliyekuwako hata kabla atomi katika...au hewa ya kuunda atomi. Hiyo ilikuwa...Ona, Yesu alisema, “Unitukuze Mimi, Baba, kwa utukufu ule niliokuwa nao pamoja Nawe kabla ya ulimwengu kuwako.” Ona, kule nyuma mbali kabisa.

32 Sasa, katika Yohana Mt. 1, Yeye alisema, “Hapo mwanzo kulikuwako Neno.” Na kwanza... “Naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu.” Mungu akijifunua Mwenyewe, akawa wanadamu. Sasa tazama jinsi alivyolifanya hilo.

33 Sasa, nyuma kule, basi, hii duara ya mwanga ilipokuja. Sasa, bado hatuwezi kuona kitu cho chote, bali kwa macho ya kimbinguni twaona ile duara ya mwanga pale. Sasa, hiyo ni Mwana wa Mungu, Logos. Sasa naweza kumwona Yeye akicheza hapa na pale kama mtoto mchanga, mbele ya mlango wa Babake, pamoja na Milele yote. Ona? Na sasa, ndipo katika mawazo Yake Yeye aanza kuwaza kuhusu vitu ambavyo vingekuwapo, na naweza kumsikia akisema, “Iwe nuru.”

34 Naye alipofanya vile, atomi ikajitokeza na jua likaweko. Likazunguka kwa mamia ya mamilioni ya miaka likifanya mavi ya chuma, na kuwaka na kuumbika kama li-lilivyo siku hizi; bado lingali linawaka, bado lingali linavunja atomi. Kama bomu ya atomiki ikilipuka, mfululizo wa atomi unge...dunia hii ingekuwa kama jua, kule, ikipasuka tu na kulipuka. Kama ungalisimama katika sayari nyingine na uitazame hii, ingalionekana kama jua lingine, ambapo atomu zile zilikuwa ziki—zikichoma dunia hii, kama haya mafuatano yangaliachiliwa kamwe na yaanze kuzunguka, kuzunguka mbio hivyo. Miali hii mikubwa hufikia mamilioni na mamilioni ya maili ya bilioni za kipimo cha joto, ya—ya—ya joto litokalo kwenye jua hilo.

³⁵ Sasa, tazama hili sasa. Nzuri! Sasa, Yeye aliumba jua. Na ndipo, muda si muda, kipande kikubwa kilipasuka kwake, kilikuwa na uzani wa karibu... karibu tu kama dunia hii, kikaenda “piii!” Ndipo Logos hii hapa sasa, Mwana wa Mungu, anakitazama, Yeye akiacha kianguke kwa miaka milioni mia ndipo akisimamisha. Ndipo kine chapasuka, Naye akiachilia (kinapeperuka) kinaanguka kwa mamilioni ya miaka, ndipo akisimamisha. Sasa, tunasimama, tukiona kikiwepo.

³⁶ Sasa, Yeye ana kitu fulani mawazoni Mwake, Naye anafanyaje? Anaandika Biblia Yake ya kwanza. Bibilia ya kwanza ambayo mwanadamu aliwahi kutazama ilikuwa nyota, zile ishara za nyota. Na ni kamilifu... tu... Ilingana na Biblia hii hapa. Inaanza, nyota ya kwanza kwa nyota zile za ishara ni bikira. Sivyo? Ya mwisho ya zile nyota za ishara ni ipi? *Leo*, yule simba. Huko ni kuja kwa kwanza Kwake Yesu, Yeye alikuja kwa bikira; mara ya pili, Yeye aja kama simba wa kabila la Yuda. Ona? Ameyafafanua wazi, ule wakati wa cancer, na kadhalika, kuendelea kote kote. Sasa, Yeye aliweka hizo zote angani mahali panapofaa. Na hivi vyote, vimwondo, vipande vya ardhi, au jua, vinavyoning’inia hapa.

³⁷ Sasa, sayansi iendepo kutafuta hayo makombora yanayoanguka, hilo halimpingi Mungu, hilo laithibitisha kwangu. Ona. hilo laifanya halisi zaidi. Sasa, basi tazama, haya makombora yote yananing’inia kule mbali na lile jua lenye joto, na kupita kule angani, bila shaka, yamekusanyika. Na muda si muda, ilianza tu kama kilima cha barafu.

³⁸ Sasa, hiyo ilikuwa dunia hii ikiumbika, kipande kikubwa tu cha makaa kilipasuka kule. Chini yake sasa si kitu ila volkeno ipasukayo na inayungua, kabisa, hulipuka, na vingine vyavyo ni vya kivolkeno. Na sayansi inadai kuwa—kuwa dunia hii, ganda lililo juu yake, tunakoishi, ni kama tu ganda la tofaa. Na yote ile... Sasa, ina mzunguko wa maili elfu ishirini na tano, labda ni unene wa maili elfu nane (hiyo ingekuwa na unene karibu maili elfu nane). Na waza tu, ndani mle, ni volkeno inayungua.

³⁹ Na theluthi mbili ya dunia, zaidi ya theluthi mbili, imo majini, na theluthi moja yayo ni nchi kavu, karibu theluthi moja. Na hebu waza tu kuhusu hili ganda ngumu tunaloishi juu yake, limejaa vitu hatari vilipukavyo, gesi, petroli, mafuta, kila kitu. Sivyo? Na theluthi mbili yake, zaidi ya theluthi mbili yake, maji. Nini maandishi ya kisayansi ya maji kwa kufupi? Sehemu mbili za hewa ya hyrodeni na sehemu moja ya hewa ya oxygeni, vitu vinavyolipika.

⁴⁰ Kuna nguvu za umeme zinazotosha katika kila chumba kutenganisha moto kwa baridi, na inaweza kufanya nguvu za umeme zitoshazo kulipua chumba. Unaweza kuweka atomi za kutosha ndani ya mpira wa golfu ilipue New York yote isiweko

usoni mwa nchi. Na ndipo wanadamu, wanaoketi juu ya mtungi wa kuzimu, wanajigongagonga kifuani na kudharau Neno la Mungu, na kusema, “Hamna kitu kama kuzimu.” (Nimeandika hilo hapa mbele kidogo, nasi tatalifikia, ona) Unakalia mtungi mkubwa wayo kila siku. Na uwapo hapa unaketi juu papa hapa, na kuzimu ku chini yako.

⁴¹ Basi sasa tazama, lakini sasa wakati hili lilipopatwa kwanza, wakati Yesu... Sasa tazama ile duara ya mwanga kule. Sasa naweza kuiona ikiondoka kuja katika dunia hii na kukaa juu yake na kuanza kuisogeza juu hapa karibu na jua. Si kitu ila mpira mkubwa wa barafu. Na ulipoanza kuyeyuka, ndipo mto mkubwa wa barafu ukaanza kuvunja huko nchi za kaskazini na kutelemka. Na ulipofanya hivyo, ukakatiza Kansas na Texas na mahali pale pote kule, na kuendelea hadi katika Ghuba la Mexico. Na muda si muda, mwajua, kitu hicho chote kilifunikwa na maji.

⁴² Ndipo, sasa tunaingia katika Mwanzo 1, tunaenda kwa Biblia sasa, kutoka kwa picha yetu ya Biblia. Mwanzo 1, “Nayo nchi ilikuwa ukiwa, tena utupu; na maji yalikuwa juu ya uso wa vilindi vya maji.” Sivyoy? “Na Roho ya Mungu ikatulua juu ya uso wa maji.” Sasa, Yeye alitenga maji, akainua milima na nchi kavu na kadhalika; akaikausha. Mimea na kila kitu, Yeye aliviumba. Naye akaumba mwezi. Na kuweka mipaka yake, ya bahari, ili isipite.

⁴³ Yeye alivileta vitu hivyo vyote pamoja, akaumba...?... Akaviumba vitu hivyo vingine vyote, wanyama wote, ndege, na nyuki, na nyani na vyo vyote vile, akaviweka vyote hapa duniani. Na ndipo Yeye akauliza swali hili sasa. “Na tu—” (Nani? Baba na Mwana) “fanye mtu kwa mfano Wetu.”

⁴⁴ Sasa, kama mtu aliumbwa kama Nuru ile takatifu kule, au kitu kama hicho, hangeonekana, (ambacho ni Kiumbe cha kiroho). Yeye alijidhihirisha au alijifunua Mwenyewe zaidi kidogo, kufanya utatu Wake Binafsi wa Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Na hapa kulikuwa na Mungu, akijifunua Mwenyewe sasa, chini hata, “na tufanye mtu,” ambaye alikuwa mwanawe, uzao uliotoka Kwake, “mtu kwa mfano Wetu,” yeye alikuwa kiumbe cha kimbinguni. “Atawale wanyama wa makondeni, na kadhalika.”

⁴⁵ Sasa, mtu yule alimwongoza mtu... aliongoza wa— wanyama na kila kitu, kama tu Roho Mtakatifu amwongozavyo mwamini halisi na wa kweli siku hizi. Sauti ya Mungu nje pale... Samahani, sauti ya mwanadamu ingenena na kusema... kuwaita ng’ombe *huku*, kuwaita kondoo waje katika malisho *haya*, kuita samaki waje kwa maji *haya*. Ona, yeye alikuwa na mamlaka, kila kitu kilimtii.

⁴⁶ Naam, walakini hakukuwa na mtu wa kuilima ardhi, Mwanzo 2, hapana mtu wa kuilima ardhi, “Na ndipo Mungu

akamfanya mtu” (Mwanzo 2:7) “kwa mavumbi ya ardhi.” Sasa tunalifuata, Yeye alimfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, na kuweka hii Roho ya kimbinguni . . .

⁴⁷ Sasa, yeye alikuwa amekaa pale. Naweza kuwa na mifano mingi yake. Naweza kumwona Adamu akisimama . . . Na tuchukue hivi, tumwone akisimama kama mti. Mungu alikuwa amemfanya. Yeye alikuwa mtu awezavyo kuwa; vidole vyake vya miguu, kama mizizi, vimejishikilia ardhini. Na Mungu akasema, “Iwe,” au akampulizia pumzi ya uhai, naye akaruka, akazinduka. Yeye alikuwa . . . Akampulizia pumzi ya uhai ndani yake, yeye akawa nafsi hai. Sasa, yeye akaanza kusonga mbele, kosonga mbele.

⁴⁸ Na ndipo Mungu akatoa ubavuni mwake sehemu yake, ubavu, na akamfanya mwanamke. Sasa, yeye alipata wapi ile roho, mwanamke? Ona? Yeye alipo . . . Mwanzo 1:26, Yeye alisema, “Na tufanye mtu kwa mfano Wetu, kwa sura Ye—Yetu, Yeye akawaumba (mtu) mwanamume na mwanamke.” Yeye alifanya roho jasiri kwa mwanamume; akaifanya ile roho oga, ndogo, dhaifu, roho ya kike kwa ajili ya mwanamke.

⁴⁹ Na unapomwona akitenda kama mwanamume, yeye ametoka mahali pake, mwaona, hapo mwanzo. Ona? Vema. Yeye apaswa . . . Nadhani ni aibu kwamba wanawake wamepoteza uzuri wao, mahali pa kike. Ni fedheha. Nawaambieni, ni aibu. Ni . . . Mwajua, naenda kusema hili. Sasa, sineni kuhusu—ninyi wanawake hapa. Lakini, hakika, kama laumiza, lafanya hivyo tu. Lakini, tazama, hebu niwaulizeni jambo fulani. Ilikuwa ya kuwa wanawake walikuwa wa kike sana hata mwanamume alipoongea nao waligeuka rangi ya uso kwa haya. Haaa! Kugeuka rangi uso kwa haya ni nini, haidhuru? Sijakuona kwa muda mrefu hata singejua ilikuwa nini kama wanawake fulani waligeuka rangi uso kwa haya. Hawana yo yote ya heshima hiyo tena, hiyo yote pale roho nzuri ya kike. Wamekuwa tu . . . Wanaweza . . . watavalia mavazi kama wanaume, wakate nywele zao kama wanaume, wavute sigara kama wanaume, walewe kama wanaume, wapige kura kama wanaume, wafanye kazi kama wanaume, hivyo basi, wanakuwa waparuzi, wajasiri. Ee, jamani! Hilo laonyesha mlipofikia. Naam hasa.

⁵⁰ Huo uwanawake mdogo, humwoni yeye tena, ni vigumu kumpata. Sivyo? Naam, hilo ni kweli. Kwa hivyo mwanamke hapaswi kusimama na kutenda kama mwanamume, mkubwa na mwenye maungo, kwa sababu yeye ni wa kupendeza. Mungu alimfanya hivyo. Naweza kuthibitisha hilo kwa Maandiko. Naam bwana. Hiyo ni kweli. Na . . .

⁵¹ Lakini, bila shaka, tunaenda nje ya swali hili, lakini sitaki mengi sana nje ya swali hili. Lakini, ona, hapo ndipo Yeye alimwumba mtu Wake wa kwanza, alikuwa kwa mfano Wake.

⁵² Na ndipo Mungu, kabla hata hakujapata kuwepo nyota, alijua kuwa dunia hii ingekuwapo. Na Yeye alijua kuwa kungekuwako William Branham akihubiri hapa mimbarani, nawe ungekuwa *John Doe* unayeketi pale ukiisikiza, kabla ulimwengu haujapata kuanza. Haleluya!

⁵³ Sasa, hapo ndipo watu wakati mwingine, katika wale—wale washikilia sheria Wakalvani, hutatanishwa kabisa. Ona? Wao husema, “Mbona wengine walichaguliwa tangu asili wapotee?” Mungu hapendi ye yote apotee. Yeye hataki hata mmoja apotee, bali, akiwa Mungu, Yeye alijua kunao wengine ambao hawataikubali. Ona? Ona, Yeye ana... ilimbidi kujua mwisho tangu mwanzo ili awe Mungu. Sivyo?

⁵⁴ Kwa hivyo Yeye alijua atahitaji wanawake, kwa hivyo akaumba roho zao papo hapo. Biblia ilisema Yeye alifanya hivyo, katika 1 Mwanzo 1:26, “Yeye alimuumba mtu, mwanamume,” katika umbo zitakazokuwepo, “mwanamume na mwanamke.” Amina. Ona? Katika umbo zitakazokuwepo, Yeye aliwaumba mwanamke na mwanamume kabla wao hawajafanywa bado kwa mavumbi ya ardhi.

⁵⁵ Na ndipo Mungu akamfanya mtu, si kwa mfano Wake. Mwili huu si wa mfano wa Mungu, mwili huu uko katika mfano wa wanyama.

⁵⁶ Je nivue koti langu? Kunakuwa joto juu hapa. Nimevaa shati lililoraruka, lakini hamtatambua hilo. Mbona, ni... Jesse hakuja kuchukua nguo zikavuliwe, kwa hivyo... Lakini, tazama, tuko kwa somo hapa sasa lenye manufaa zaidi ya shati lililoraruka mimbarani. Sivyo? Lamaanisha Uzima wa Milele.

⁵⁷ Sasa, tazama mtu. Mungu alijua hapo mwanzo kuwa angekuwa na wanaume na wanawake. Yeye alijua ya kwamba Mwokozi angekuwa hapa na ingembidi Yeye amlete Yesu, Naye angesulubiwa. Na Yesu aliwaambia wanafunzi Wake, alipokuwa hapa duniani, kuwa Yeye “aliwajua hao hata kabla ulimwengu kuwekwa misingi,” kabla ulimwengu haujapata kuwepo.

⁵⁸ Na Mungu alisema, pia au Paulo akinena, katika Wagalatia, alisema kuwa, “alituchagua sisi na kutuita katika Yeye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.” Wazia hilo! Kwamba Mungu... Kunaye ye yote ambaye angependa kusikia Maandiko yasemavyo kuhusu hilo, inueni mikono yenu. Lalingana moja kwa moja na swali hili. Fungueni pamoja nami katika Wagalatia, sura ya 1. Sikiza hapa. Sikusudii Wagalatia, nakusudia Waefeso. Sikiza kwa makini sasa yale Mungu alisema, Waefeso 1:

Paulo, mtume wa Yesu, kwa mapenzi ya Mungu; kwa watakatifu walioko Efeso, wanaomwamini Yesu Kristo.

Neema na iwe kwenu, na amani zitokazo kwa Mungu Baba yetu na kwa Bwana Yesu Kristo.

Atukuzwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo aliyetubariki kwa baraka zote za rohoni, katika ulimwengu wa roho, ndani yake Kristo Yesu:

59 Sasa, liko hapa, tazama:

Kama alivyotuchagua katika yeye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, . . . (whiu!)

60 Hilo ni nzuri sana. Sivyoy? Hilo ni nzuri sana, hilo ni bora sana! Kabla kuwepo misingi ya ulimwengu, Mungu alimjua Orman Neville na kujua kuwa yeye angehubiri Injili. Si ajabu hiyo? “Alivyotuchagua . . .” Naam, yeye ni mshiriki wa Kanisa, na Mungu alijua Yeye angekuwa na Kanisa hilo. Naye alisema, Paulo akiliambia kanisa la Efeso, alisema, “Alivyotuchagua katika Yeye.” Sasa, sote tu washiriki wa Mwili wa Kristo. Sivyoy? Na Mungu, kabla kuumbwa kwa ulimwengu, alinichagua mimi na wewe katika Yeye kabla ulimwengu haujapata kuumbwa. Whiu! Lo! Si ajabu hiyo?

61 Sasa, mtu wa kwanza basi, Yeye alimuumba yule mtu wa kwanza katika mfano Wake nasi tunarudi tena kwa mfano huo, naam, kwa mfano wetu wa kwanza tulioumbiwa.

62 Mungu aliponiumba mimi, William Branham, nilikuwako kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, Yeye aliumba utu wangu, roho yangu. Sikuwa na ufahamu wa lo lote kwa kadiri nijuavyo, lakini ile . . . Nilikuweko. Ee, si—siamini mnalipata. Lakini sasa, kwa dakika moja hivi, Yesu aliwaambia wanafunzi kuwa Yeye “aliwajua wao kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu,” na Paulo alisema hapa kwamba “Alivyotuchagua katika Yeye kabla ulimwengu haujaanza bado.” Naam, kulikuw—ako na sehemu yangu, Orman Neville, na ninyi wengine wenu wote hapa, mlio katika Kristo Yesu kabla ulimwengu haujapata kuanza. Na huu ndio mchanganuo wangu wa hilo. Nadhani kuwa watu siku hizi wenye Roho huyu, au yule roho, sehemu ya hivi viumbe vya kimalaika, roho hizi zilizozunguka-zunguka karibu na Mungu, amabazo hazikuanguka mwanzoni na ziliupinga aongo wa Ibilisi Mbinguni.

63 Na theluthi mbili ya dunia imo dhambini, na zaidi ya hiyo, ambapo theluthi mbili za malaika zilifukuzwa. Na hizo roho za pepo huwaingia watu na kupata makao miilini mwao. Mwafahamu lile ninalokusudia? Ni pepo ambao wakati mmoja . . . wakati mmoja walikuwa hai nao wakawaingia watu na kuwapa tabia fulani. Yesu alitoa saba ya hao toka kwa Mariamu Magdalena. Kiburi, majivuno (watu wakubwa, mwaona), uchafu, unajisi, utovu wa adabu, maigizo, mashindano. Vitu hivi vyote, ona.

64 Hizo ni roho zilizoumbwa nyuma kule Mungu alipoanza kumwumba mtu kwa mfano Wake. Aliviumba hivyo viumbe vya kimbinguni, pepo hao.

⁶⁵ Na ndipo Yeye akamweka mtu katika mavumbi ya ardhi, ambaye alikuwa mtu wa kwanza, Adamu. Na mtu huyo aliumbwa kwa mfano, huyu mtu mwanadamu hapa, amefanywa kwa mfano wa wanyama. Hii miili ya kibinadamu imefanywa kwa mfano wa wanyama.

⁶⁶ Tuna mkono kama tu wa nyani, na—na tuna mguu kama wa dubu. Chukua mwana dubu mdogo, mchune ngozi, mchune ngozi ukamsimamishe karibu na msichana mdogo na uone, tofauti yake. Heehe! Ndugu yakubidi hakika utazame kwa makini. Kiwambo chote cha moyo, maumbo, ni karibu sana kuwa sawa, jinsi alivyofanywa na maumbo yake, na kila kitu vivyo hivyo hasa. Ni katika mfano wa wanyama kwa sababu yeye alifanywa kwa asili ya mnyama, kwa sababu huo ulikuwa wajibu wake kuwaongoza wanyama.

⁶⁷ Na umwondoe Roho Mtakatifu kwa mwanadamu, yeye yu chini zaidi ya mnyama, yeye yu mbaya zaidi ya mnyama. Hilo ni jambo nzito kusema. Lakini mchukue mtu asiyezaliwa mara ya pili katika nia yake, asipokuwa na Roho Mtakatifu kuongoza mawazo yake, na—na mambo kama hayo, yeye angemtupa mtoto toka mikononi mwa mamake na amnajisi mama huyo kwa ajili ya tamaa mbaya ya kinyama. Naam hasa.

⁶⁸ Na mwanamke asiye mwema. Umchukue mama nguruwe mkongwe au mbwa mzee, tungempa kila aina ya majina kwa ajili ya . . . Lakini audilifu wake ni kwa ajili ya kujipatia watoto wake, na yule nguruwe kwa kujipatia watoto wake, lakini mwanamke mkaidi na mwenye sifa mbaya ni kitu tu. . . mchafu tu wakati wote. Naam, kwa hivyo kumbuka, kuwa wewe u . . . bila Kristo, uadilifu wako u . . . unaweza kupungua zaidi ya wa mbwa. Naam.

⁶⁹ Mbwa hana haja ya kuvaa mavazi kujisetiri, hakuna mnyama mwingine ye yote. Ni mwanadamu aliyeanguka, si mnyama. Lakini wanyama chini ya mwanadamu (ubinadamu), walikuwa chini yake kwa sababu mwanadamu alikuwa kiongozi wake na kiongozi wake mkuu. Na kila mnyama kondeni anaogopa mwanadamu.

⁷⁰ Mtu fulani alikuwa akiniuliza mimi, wakati fulani, kuhusu kuwinda, “Je, unakuogopa”. Hasha, kila mnyama aliyewahi kuumbwa aogopa mtu, kwa sababu hilo ni tangu mwanzo nyuma kule. Ona? Hakika, ukikimbia atakukimbiza, naam, au mbwa au ye yote umtakaye. Vema.

⁷¹ Lakini sasa, tazama sasa, huyo mwanadamu alipokuja chini hapa . . . Sasa tazama hapa . . . Wasema, “Naam, na hilo je, Ndugu Branham?”

⁷² Sasa, hapa unamkuta Mungu ndani kabisa, na kati ya wale wa umoja na wa utatu mtapata kitu kile sawasawa hasa sasa. Sasa tazama! Mungu alipojishusha, alipojifunua Mwenyewe, alijifunua hata akafikia mtu huyu. Sasa, mwanadamu alitenda

dhambi si katika roho yake, lakini kwa mwili wake, tamaa mbaya, ashiki. Ndipo yeye alipotenda dhambi, alijitenga mwenyewe na Muumba wake. Na ndipo Mungu, yule Logos, yule aliye Muumba wake, alishuka chini na akafanywa kwa mfano wa mwanadamu. Mwanadamu aliumbwa kwa mfano wa Mungu, halafu akafanywa kwa mfano wa mnyama, naye akaanguka. Naye Mungu akashuka chini kwa mfano wa mwanadamu, katika Mwanadamu Kristo Yesu, aone maumivu. Mungu asingeona maumivu katika Roho. Angeonaje maumivu ya mwilini katika Roho? Hangeweza. Kwa hiyo Mungu akajifunua Mwenyewe na akafanywa kwa mfano wa mwanadamu, kumkomboa mwanadamu aliyepotea. Ona?

⁷³ Na ndipo Mungu akateswa katika mwili. 1 Timotheo 3:16, “Na bila shaka,” hilo ni ubishi, “siri ya utauwa ni kuu. Mungu alidhihirishwa katika mwili, akaonekana na malaika, akahubiriwa, akasulubiwa, akaaminiwa, na akachukuliwa juu kwenye mkono wa kuume wa Baba.” Sivyo? Mungu Mwenyewe alishuka chini na kukaa katika mwili wa kibinadamu na akapata majaribio. “Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi Yake.” Mwaona jinsi upendo ulivyo? Upendo wa Mungu!

⁷⁴ Basi, sasa, nadhani hilo lingempata huyo, *mwanamume* na *mwanamke*. Sasa, mwanamke ni... Hebu nilipate hili vizuri sana ili mweza kuliona, ona. Mwanamke ako chini ya mamlaka ya mumewe. Na Biblia ilisema kuwa, “Mwanamume yambidi amtawale mkewe.” Lakini jinsi wamegeuza hilo! Mwanamke anamtawala mwanamume, “Sasa, wewe kaa nyumbani, Yohana! Huendi!” Na hilo latosha, “Naam, mpenzi wangu.” Ona?

⁷⁵ Lakini hebu nikwambie kitu fulani, bwana. Utahukumiwa kwa ajili ya mkeo, lakini mkeo hatahukumiwa kamwe kwa ajili yako. Wewe u kichwa cha mwanamke huyo, na Mungu ni kichwa cha mwanamume. Kwa hivyo Yeye alisema, “Na mwanamume akate nywele zake kwa ajili ya Kristo. Na mwanamke awe na nywele zake, maana akizikata nywele yuaibisha munewe.” Ona? Mwaona ninachomaanisha kwa yale Maandiko yasemavyo?

⁷⁶ Nilikuwa na moja moto moto, chini kule siku moja kule Shreveport. Wao wanaongea kuhusu wanawake, na yabidi wawe na nywele ndefu. Nami nilisema, “Mwanamke aliyefupisha nywele zake, mume wake ana haki na ruhusa ya Biblia kumtaliki.” Naam. Hivyo ndivyo Biblia ilisema. Naam hasa. Jamani! Wanawake waliojazwa Roho Mtakatifu wakiketi pale, jinsi tu walivyofundishwa, hivyo tu. Ona? Naam, juu juu tu. Na kama...

⁷⁷ Yeye alisema, “Sasa, kama wangeikata, kama kuna kitu fulani kasoro ikawabidi wakate nywele zao,” kasema, “na wachukue wembe na kuinyoa yote na afanye nywele zake fupi mno.” Heri uje hivyo. Naam. Hivyo ndivyo Maandiko yalisema.

Kisha inasema, “Akikata nywele zake, yuaaibisha mumewe. Na mwanamke asiye na heshima kuna sheria halali ya kumtenga na kumtaliki.” Lakini, mwanamume yule hawezi kuoa tena, sasa. Lakini yeye—lakini yeye aweza kumtaliki. Naam. Hayo ni Maandiko. Ee ndugu, kile tunachohitaji ni usiku wa maswali! Naam. Hilo ni I Wakorintho, sura ya 14 mkitaka kuisoma. Vema. Sasa, hilo—hilo. . . Sasa mwanamke huyo.

⁷⁸ Mungu—Mungu alimuumba mtu, mwanamume na mwanamke. Mwaona kile Yeye alichofanya? Akamuumba huyo mtu. Alimuumba. . . Sasa, hilo ndilo swali la kwanza, ona, “Aliwaumba,” na mengineyo, Mwanzo 1:26. Mwanzo 2:7, “Akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, akampulizia puani.”

Nini tofauti, au—au uko wapi uhusiano katika Maandiko haya yaliyo juu hapa? Kuna uhusiano gani kati ya mtu wa kwanza na mtu wa pili?

⁷⁹ Yule mtu wa kwanza ndiye yule wa pili amedhihirishwa katika zile hisi tano. Ona? Sasa hivi huwezi—huwezi kumgusa Mungu kwa mikono yako *hivi*, huwezi kumwona Mungu kwa macho yako. Yeye hakukupa hizo ufanyie hilo. Wewe u. . .

⁸⁰ Je, mliwahi kusikia mtakatifu mzee akifa, wanaposema, “Huyo ni mama, sijawahi kumwona kwa miaka mingi”? Mliwahi kusikia hayo wakati watu. . .? Ona, jambo ni kwamba macho hayo yanafifia na macho ya kiroho yanaingia. Ona? Na ndipo wakati mwingine tunapo. . . Mungu akifanya. . . Twaona maono ambapo macho ya kawaida yanafifia. Papo hapo mbele zetu, tunatazama moja kwa moja, na pale kuna ono mbele yetu likionyesha mambo ya kimbinguni ya Mungu. Mwafahamu ninalomaanisha?

⁸¹ Kwa hivyo basi, tazama, “Maskani hii iliyo ya dunia hii. . .” Sasa, baadhi yenu wanawake na wanaume hapa mnazeeka. Tazama, “Hii iliyo ya dunia hii. . .” Nawaza kuhusu baba mzee pale, umri wa miaka tisini na miwili. “Nyumba ya maskani yetu iliyo ya dunia hii ikiharibiwa, kuna mtu wa rohoni, mwili wa rohoni unaotungoja usioweza kuangamia.” Nitakutana nanyi kule. Nitatembea kule. . .

⁸² Siwezi kumgusa Ndugu Neville ndani—ndani mle, kwa sababu Yohana aliziona hizo nazo zilikuwa roho chini ya madhabahu, zikilia, “Hata lini, Bwana, hata lini?” Mwajua sababu yake, tulisoma Ufunuo wote. Na jinsi ndani mle wanatamani warudi na kuvikwa miili yao inayokufa. Walikuwa wakilia, “Hata lini, Bwana?”

⁸³ Naam, walijuana wao kwa wao, lakini hawangeongea na kusalimiana kwa mkono, au kunradhi. . . wangeongea, bali hawangesalimiana kwa mkono na kadhalika. Hapa kuna mfano kulithibitisha hilo. Wakati yule mchawi wa Endori alipoita roho ya Samweli, na Sauli akamtazama na kumtambua kuwa Samweli. Na Samweli alimtambua Sauli na kusema,

“Mbona umenitaabisha mimi, hata kunipandisha juu? Kwa kuwa umekuwa adui wa Mungu na Bwana amekuacha!” Sivyo? Na pale kasimama mzee Samweli amevalia joho lake la kinabii, naye akamtazama. Yeye alikuwa katika roho.

⁸⁴ Yule mchawi alimwona na akaanguka ardhini, kasema, “Naona miungu wanatoka katika nchi.”

Yeye alisema, “Mbona umenitaabisha mimi?”

Yeye alisema, “Vema nataka kujua vita vitaendeleaje?”

⁸⁵ Kasema, “Kesho utakufa vitani, na wanao pia, kesho wakati kama huu utakuwa pamoja nami.” Ona? Sasa, yeye alikuwa na fahamu, naye alionekana tu kama yeye alivyokuwa alipokuwa duniani, kwa huyo mchawi aliyekuwa amesimama, akimtazama, na Sauli.

⁸⁶ Sasa, tazama. Wakati mwingi... Vipi basi, na baba au mama walipokuwa wakifa na wakawaona wapendwa wao wamesimama pale? Waliwatambua. Lakini ni katika mwili ule wa kimbinguni.

⁸⁷ Lakini sasa hapa kuna sehemu yenye fahari. Katika kule kurudi kwa Yesu katika ufufuo, hautakuwa mwili huo. Mwili huo basi, hicho kiumbe cha kimbinguni alichokiumba Mungu mwanzoni, hicho kitarudi duniani kuchukua mwili mwingine, usiozaliwa kwa mwanamke, bali ulioubwa na Mungu (Haleluya!), hautazeeka kamwe wala kupata kunyanzi, hautakuwa na mvi kamwe kichwani mwako. Kuwa mkamilifu, milele! Haleluya! Ewe ndugu, hilo lingenifanya nipaze sauti katika usiku wenye joto! Naam! Ee, hili vazi la mwili nitalitupa, na kufufuka na kupokea thawabu ya milele! Tuhangaishwe na nini jamani?

⁸⁸ Pale kuna mpango wote amewekwa pale, jinsi Mungu alivyoniumba mwanzoni. Nilikuja hapa duniani, nikachukua mahali pangu kama Mhubiri wa Injili, au wewe kama mwanamume au mwanamumke kuingia wokovuni, ndipo utaishi maisha hayo kwa neema ya Mungu. Haleluya! Na Roho yule yule anaondoka hapa aliyekuwepo nyuma kule mwanzoni. Nitarudi nyuma kwa fahamu za kujua nimekuwa hapa, (Haleluya!) Na ndipo ningoje pale chini ya madhabahu, nimebarikiwa milele, katika raha. Na ndipo nitakaporudi tena, nitauchukua mwili wangu katika uzuri wake wa hali ya juu zaidi, kabla kifo hakijapata kuuguza.

⁸⁹ Mauti hukugusa wewe unapofikia umri wa miaka ipatayo ishirini na miwili au ishirini na mitatu, unaanza kufifia. Wewe siye mwanamume uliyekuwa na siye mwanamke uliyekuwa, baada ya kufikia karibu ishirini na mitano, kitu fulani kinaingia. Makunyanzi yanaanza kuja chini ya macho yako. Huwezi kuona kama ulivyokuwa ukifanya. Thelathini, unaweza kuitambua zaidi sana. Ngoja hata ufikie arobaini na minne kama mimi, na ndipo unaitambua zaidi sana. Lakini, Ewe ndugu! Ngoja

hata nifikie themanini, tisini, na kwa mkongojo huo, nikisimama pale. Ni nini? Mungu anamweka tu mbioni kukimbia. Lakini siku moja yenye fahari. . . Hicho ni kifo kikiingia.

⁹⁰ Mimi wakati mmoja nalikuwa na mabega yaliyonyoka, na nalikuwa na nywele nyeusi (na kichwa kilichojaa nywele), na bila makunyazi chini ya macho yangu; naam mnitazame, sasa, najikunyata, mabega yamejikunyata, naanza kunenepa, na mikunjo chini ya macho yangu, mwenye upara. Mbona, tazama yale kifo kimenitendea katika miaka ishirini iliyopita. Kifo kinafanya hayo. Subiri hata nifikie themanini, Mungu akinijalia kuishi, na mtazame nitakavyokuwa, nikisimama hivi kwa mkongojo, nikitetemeka-tetemeka hivyo mahali fulani. Lakini haleluya, siku yenye fahari, kifo kitauchukua mwili wote. Ndipo nitakapofufuka katika ufufuo nitakuwa vile nilivyokuwa, jinsi Mungu alivyoniumba hapa duniani nilipokuwa mzuri sana, katika mwili usiofanywa na Bi. Branham na Bw. Branham, lakini uliombwa na Mungu Mwenyewe; huru kwa majaribu, huru kwa dhambi, huru kwa kila kitu kinginecho, usiokuwa na ugonjwa kamwe, kuvunjika moyo. Jamani!

⁹¹ Ndipo nitashika mikono ya maskini mke wangu mpendwa na kutembea katika Paradiso ya Mungu hivyo, wapya. Utafanya vivyo hivyo. Si yue mwanamke mkongwe mwenye mvi unayemwongoza hapa na pale usiku huu, ukimwita mke wako, lakini yeye atakuwa tu mrembo kama alivyokuwa siku ile uliyomwoa pale madhabahuni. Haleluya! Whiu! Hayo yatosha kumfanya mtu apaze suati. Sivyo? Ona?

⁹² Vema, huo ndio uhusiano. Mungu ameazimia. Mungu akatapo kauli kufanya lo lote, sharti liwe. Shetani aliharibu mfano huu kwa tamaa ya kujuana kimwili, kwa mwanamke, kuzaa watoto. Yeye aliuharibu. Lakini endelea nao, ni sawa. Makao haya yatachukua haya, kwa sababu jambo pekee unalofanya katika maisha haya ni kuchukua mfano wako na sura, jinsi ulivyo. Kama wewe una nywele nyekundu sasa, utakuwa na nywele nyekundu wakati huo. Kama wewe una nywele nyeusi sasa, utakuwa na nywele nyeusi wakati huo. Ona, vile ulivyokuwa ulipokuwa na nguvu zako zote za ujana. Na uki. . . Shetani aliharibu mfano ule, hata hukupata. . . kile Mungu alichonua wewe uwe, utakuwa. Ee, tukufu vipi! Huyo ndiye mtu wako.

⁹³ Sasa Mwanzo 2. Aisee, yanibidi niharakishe, nitayapata. (Una kitu fulani ulicho nacho? Ulitoa. . . una ya kujibiwa?) Vema, Mwanzo 2:18-21:

2. Mungu alimfanya Hawa kwa ubavu wa Adamu, Mwanzo 2:18-21. Je, Mungu alimuumba mwanamume na wanawake, ndipo akawafanya Adamu na Hawa—Hawa?
3. Na je, Kaini alienda kwa viumbe halisi wa mwanamume na mwanamke ampate mke wake?

⁹⁴ Basi, hebu sasa...si...Mtu huyu labda yumo hapa aliyeandika haya. Sasa, Mungu alipo...Katika swali la kwanza hapa:

Je, Mungu aliwaumba mwanamume na wanawake, wa Mwanzo 2:18-21?

⁹⁵ La. Ni-ni...kama—kama mtakavyoona hapa, 2:18-21 sasa, tazama:

BWANA Mungu akasema, Si vema...huyo mtu awe peke yake, nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye.

BWANA...akafanyiza kutoka katika ardhi...kila mnyama... na kadhalika.

⁹⁶ Sasa, Mungu alimfanya Hawa toka ubavu wa Adamu. Mwanamke ana ubavu mmoja zaidi siku hizi katika maumbile na umbo lake kuliko mwanamume, kwa sababu ubavu ulitolewa kwa mwili wa Adamu. Adamu alikuwa tayari amekwisha kufanywa na alikuwa akiishi, na alikuwa mpweke, na ndipo Mungu alisema, “Si vema mtu awe peke yake.”

⁹⁷ Kwa hivyo hawa makasisi na wengineo wanaonyimwa haki ya kuwa na mke. Sasa, hilo, kanisa la Kirumi laweza kufanya lo lote...Hilo ni wao, wao ndio watakojibia hi—hilo si mimi.

⁹⁸ Vema, niliulizwa na m—mtu fulani, hivi majuzi, kasema, “Wawazaje kuhusu makasisi?” Nikasema, “Wawazaje kuhusu huyo kasisi kijana hapa mjini aliyemchukua mwanamke huyo, msichana huyo, msichana wa hapa Jeffersonville, na akaenda na kumwoa?” Katika kanisa la Ki-Irish, mwakumbuka. Nasahau jina lake lilikuwa nani.

⁹⁹ Nilisema, “Yeye alikuwa na haki ya kuoa kama nilivyo nayo. Hilo ndilo hasa ninalowaza.” Nilisema, “Jambo pekee ninaloonelea...Nadhani yeye alikosea, yeye angeenda kanisani na ajiuzulu huduma yake ndipo aende na kumwoa msichana yule, badala ya kutoroka hivyo.”

¹⁰⁰ Sasa, mwakumbuka ilipotendeka majuma machache yaliyopita hapa Jeff., yule kasisi M-Irish Mkatoliki chini hapa. Yeye ni kijana, naye alikuwa yuaenda...ana msichana mpenzi chini papa hapa. Na yeye alipokuwa...Walimpa matoleo makubwa ya hiari, kuenda kubadilishana jimbo la kasisi naye, wakampeleka Indianapolis mahali fulani. Naye akayachukua yale matoleo ya hiari, msichana na vyote akaenda na kuoa, nao hawakusikia toka kwake tena. Vema, yeye alikuwa na haki ya kuoa lakini hakuwa na haki ya kufanya hivyo. Haikumpasa kufanya hivyo. Yeye angelienda kanisani na—na kusema, “Basi, ninajiuzulu huduma hii kama kasisi. Naenda kuoa, na hilo latosha.”

¹⁰¹ Lakini, sasa, Mungu alipomfanya Hawa, na—na Adamu na Hawa kwa wakati ule ule, jambo pekee Yeye alilofanya lilikuwa la kimbinguni, Adamu wa kiroho na Hawa wa kiroho,

mwanamume na mwanamke. Ndipo yeye alifanya... alimweka Adamu ndani mle. Haikuwa vema kwa... Ona, ni picha ya Mungu akijifunua wakati wote. Kila kitu hivi, inakuja tu tu moja kwa moja, ikijifunua tu moja kwa moja, kuja kote katika ule Utawala wa Miaka Elfu kule na kuendelea hata katika Milele. Ni mfano wa Mungu tu ukijifunua, Mungu akijifunua Mwenyewe.

¹⁰² Hapa, Mungu alijidhihirisha Mwenyewe katika Kristo Yesu. Ilionyesha jinsi Yeye alivyokuwa. Yeye alikuwa nani? Mtu wa huzuni nyingi, ajuaye sikitiko, mwenye mapenzi. Kwa kahaba, “Wako wapi wanaokuhukumu wewe?”

“Sina—sina ye yote, Bwana.”

“Wala nami sikuhukumu. Ondoka uende, na usitende dhambi tena.”

¹⁰³ Mchovu na mnyonge kwa kutembea karibu maili thelathini siku hiyo, kupitia katika changarawe jangwani na mengineyo; palikuwako mwanamke kule Naini aliyetoka nje, na mwanawe wa pekee, amekufa amelazwa pale. Yeye alisimamisha msafara wa mazishi, akaweka mikono Yake juu yake, kasema, “Amka.” Na mvulana aliyekuwa amekufa akafufuka tena. Huyu—huyo ni Bwana wetu Yesu. (Asante, Teddy, mwanangu.) Na pale, huyo ndiye Bwana wetu Yesu ambaye hakuchoka sana, hakuishiwa na nguvu sana asifanye lo lote zuri. Vema.

Sasa, hapa kuna jambo lingine:

Je, Kaini alienda kwa—kwa vile viumbe vya kwanza vya mwanamume na mwanamke kuoa mke wake?

¹⁰⁴ Sasa, hapo kuna swali la kutaka uangalifu mwingi, sasa sikiza kwa makini. Sasa, eh, nina...mmeona watu wakiandika magazetini, “Kaini alimpata wapi mke?” Ee, nilikuwa nikiliuliza.

¹⁰⁵ Nami sikuwahi kudhani kuna kuzimu kunakowaka moto, kwa karibu miaka minne baada ya kuongoka kwangu. Ilinibidi nilione katika Maandiko. Kama sijui, sitasema lo lote kuhusu hilo. Ona?

¹⁰⁶ Lakini sasa, “Kaini alimpata wapi mke wake?” Sasa, hilo ni—ni uchanganuo wa swali hili sasa. “Na je, Kaini alimpata mke wake toka kwa viumbe vya mwanamume na wanawake, kumpata mke wake?” Ona? Sasa, sasa, mmoja wa wa kwanza...

¹⁰⁷ Huyu Bi. De Ark, nyote mlisikia kuhusu uponyaji wake hivi majuzi, jinsi Mungu alivyombariki na kadhalika. Yeye alikuwa amelala, akifa, walikuja yapata saa nane ya usiku.

¹⁰⁸ Na kwa hivyo sasa, hivyo ndiyo nilivyokuja...Mvulana wake, George, yule mvulana alikuwa mpiga ramli, naye Ed, pia (walirudishwa). Nami nilisikia majadili yale nyuma kule, ambapo lile la kwanza...ni wapi ambapo Kaini alimpata mke wake. Vema yule aliyekuwa jukwaani aliyeonekana kana kwamba msimamo wake ulikuwa bora zaidi, yeye

alisema, “Nawaambieni ambapo Kaini alimpata mke wake,” kasema, “Kaini alienda na akaoa sokwe mkubwa wa kike.” Na kasema, “Toka kwa huyo sokwe kukaja watu weusi.” Kasema, “Mnatambua mtu mweusi ana kichwa kama kwamba kimechongoka *hivi*, kama—kama alivyo sokwe, kichwani.”

¹⁰⁹ Vema, nilisimama pale, nilikuwa tu karibu miezi miwili katika Injili. Nilisema, “Sitaki kutofautiana nawe bwana, kwa sababu mimi si mwanachuoni, niliokoka hivi majuzi. Lakini” Nilisema “kama ni hivyo basi ule uzao wa watu weuzi ungalikoma kuwepo baada ya yale maangamizi ya ghalika, ulimwengu ulipoharibiwa kwa maji, maana Nuhu na jamaa yake ndio pekee yao waliokuwa safinani. Ni hao pekee waliokuwa safinani. Ule uzao wa watu weusi unglikoma kuwepo,” nilisema, “kama hilo ni kweli.” Nilisema, “La, bwana! Uzao wa watu weuzi haukutokea pale kamwe. La, bwana. Uzao kwa watu weusi ni wa ukoo ule ule sisi tuliotokea, na kila mwanadamu, ule ule.” Hakuna tofauti. Hakika. Sisi sote tu . . . Huenda mwingine akawa wa manjano, na mwingine wa, kahawia, na mwingine mweuzi, na mwingine mweupe, na mwingine mweupe kidogo, na mwingine mwekundu, na kuendelea hivyo, lakini ninyi nyote mumetoka kwa ukoo huo. Hiyo ni sehemu inayoonekana nje hapa. Naam. Hao ni wanadamu vivyo hivyo, walioumbwa hapa na Mungu.

¹¹⁰ Na sasa, tazama hapa si muda mrefu uliopita, nikisimama hapa na madaktari fulani katika Louisville, nilikuwa nikiongea kuhusu Afrika jinsi watu hao maskini, aina ya wala watu, hasa jinsi walikuwa na mwanamke pale, alimchukua mtoto mchanga . . . Walimpata mtoto mchanga, ambaye mwanamke yule alikuwa amempiga hivyo na kumfungia kijitini ili aoze kwa siku chache, mwajua, hadi aoze kabla hawajamla, mwajua. Kitu kama hicho, wanaacha ioze kidogo, ili iwe nyepesi.

¹¹¹ Usidhani hilo limezidi sana kwa makabila yanayokula watu. Katika Uingereza vivyo hivyo, wanaua tausi na kuwatundika mitini, Wa-Anglo-Saxon, kule Uingereza, kabila hilo. Msidhani . . . Haikubidi uende Uingereza, hebu tu nenda chini hapa katika majimbo ya kusini, utapata kitu kile kile. Hakika. Mtu ye yote anayekula konokono au—au nyoka wenye sumu, anaweza kula kitu cho chote kile. Kwa hivyo . . . Naam.

¹¹² Sasa tazama, hebu—hebu niwaambieni. Lakini, hivi ndivyo ilivyotendeka. Wale watu weusi . . . ule—ule uzao wa watu weusi hauhusikani na hili. Kaini . . .

¹¹³ Sasa, nawatakeni mtazame. Wao walisema kuwa “Yeye alienda katika nchi ya Nodi.” Sasa, Kaini alikuwa katika Edeni. Na Edeni, Bustani ya Edeni, ilikuwa mashariki ya Edeni. Sivyo? Bustani ya Edeni. Na wale Makerubi wakawekwa, na ule Mti wa Uzima ulikuwa kwenye lango la mashariki la Bustani ile, na pale ndipo nadhani Kaini na Habili walitolea sadaka yao. Na

pale ndipo ambapo hao Makerubi wenye panga zinazowaka moto hawangewaruhusu waingie tena, mashariki mwa lango lile!

¹¹⁴ Je, mlitambua, Yesu atakuja toka mashariki. Nuru hupambazukia mashariki. Kila kitu kijacho... Ustaarabu ulianza mashariki na ukaelekea magharibi, hata ukazunguka kote na kujifikia wenyewe tena. Sisi tuko katika Nusu ya Magharibi ya dunia. Huu ni wa Mashariki, Mashariki ndiyo ustaarabu wa kale sana. China ndiyo yenye ustaarabu kale sana sa ujulikanao na wanahistoria ulimwenguni siku hizi. Mashariki!

¹¹⁵ Ee, jinsi tungekawia kwa maswali haya kwa masaa kadha, kwa moja, lakini singeyafikia mengine. Lakini tazama, hapa kuna... Wangapi wangependa kujua yale tunayoamini kuhusu Kaini, wapi na nani aliyekuwa mke wa Kaini? Hebu tuone. Vema. Nitawaambieni kile Kaini alifanya, na ndilo jibu pekee lenye busara unaloweza kufikiria: Kaini alimwoa dada yake. Ilimpasa afanye hivyo maana kulikuwako na mwanamke mmoja tu duniani wakati huo; Biblia inatoa tu ushuhuda wa kuzaliwa kwa watatu, Hamu, Shemu... au la... samahani, walikuwa Kaini, Habili na Sethi. Lakini kama hakukuwahi kuwa na wo wote... Biblia ni shida kutaja kuzaliwa kwa wasichana. Mwajua hilo.

¹¹⁶ Sasa, hakika nitawapwaruza wanawake usiku huu. Lakini, tazama, ulimwengu unawaabudu wanawake, lakini wanawake walikuwa chombo cha Shetani mwanzoni. Na yule asiye haki siku hizi ndicho chombo bora zaidi alichonacho. Atawapeleka wahubiri kuzimuni kuliko vyumba vyote vya vileo vilivyoko ulimwenguni. Hebu hawara mdogo mwenye sigara pembeni mwa kinywa chake, na nywele zake zimepakwa rangi hivyo, na kope kubwa mno na refu zinazopepesa-pepesa, ndugu, kidogo... aonekana mzuri kwa maumbo yake, tazama kile atafanya.

¹¹⁷ Mhubiri, heri ujifunike na Damu ya Yesu Kristo. Naam. Sasa, usiniambie, wewe u mwanamume! Nimeona mengi sana kama hayo. Sasa, tazama hapa. Jambo bora zaidi la kufanya ni kutuliza nia yako kwa Kristo Yesu na nia yako iwe safi.

¹¹⁸ Kama Paulo alivyonena ndani mle, kasema, “Ni... Nanyi mwajua tuna uwezo wa kuchukua pamoja nasi dada. Nina uwezo kufanya hilo, lakini” kasema “sitafanya hivyo.” Ona, yeye hangefanya hivyo. Yeye alisema, “Najua kuwa huduma inapaswa kuishi kwa—kwa... Ng’ombe apurapo nafaka usimfungue kinywa.”

¹¹⁹ Mwajua sisi wakati mwingine hudhani, kwa sababu sisi tu wahubiri... (Si wewe na mimi, sisemi, ndugu). Lakini wahubiri hudhani kwa sababu wao ni wahubiri kwamba—kwamba wao ni watu wakuu kuliko mmoja wa washiriki wa kanisa. Wewe si mkuu na wewe si mkubwa zaidi machoni pa Mungu kuliko huyo mlevi aliyeongoka saa moja iliyopita.

¹²⁰ Hilo ni jambo moja yale matengenezo hayakusahihisha, ilikuwa jambo hili. Najua mimi hutia sahihihi kwa jina langu “Reverend.” Naam hasa, hiyo tu ni—ni desturi ya siku hizi, lakini haipaswi kufanywa. “Reverend,” na “Askofu” na “Daktari,” na vitu hivyo vyote vimetengenezwa na wanadamu, navyo ni upuzi! katika Biblia wao walikuwa “Petro,” “Yakobo,” “Paulo,” “Yohana,” na wengineo wote.

¹²¹ Paulo alisema “Sasa hapa najua nahubiri Injili, huo—huo—huo ni wajibu wangu.” Mimi ni mhubiri na yeye ni mhubiri, na Ndugu Neville ni mhubiri, lakini ni . . . Huo ni wajibu wetu, kuwa mhubiri. Vema, hilo ndilo litupasalo kufanya. “Lakini hebu nifanye kitu fulani,” Paulo alisema, “hilo ni zaidi ya hilo. Sasa, nina haki ya kuchukua pesa,” Paulo kasema, “lakini nitatengeneza hema kuwaonyesha ninyi ninaweza—ninaweza kujitolea.” Yeye alisema, “Ni heshima, ndoa ni jambo la heshima kwa wote, malazi ni safi. Ni vema kwa mwanamume kuoa.” Yeye kasema, “Nina haki ya kuoa. Sasa, ni—ningeo, nina haki halali kuoa. Lakini sitaoa, nataka kujitolea tena zaidi kwa Bwana.” Ona? Ndipo yeye alisema, “Kila mtu ajua wito wake. Na yeye afanye kama . . . Wengine ni towashi kwa ajili ya Neno la Mungu, na kadhalika.”

¹²² Tunataka tufanye kitu fulani mbali na wajibu wetu. Na kama umezaliwa mara ya pili hasa kwa Roho wa Mungu na unasema, “Huo ni wajibu wangu kuenda kanisani, nadhani yanipasa kwenda.” Ee, lo! Vema, nataka kufanya zaidi ya hilo, nataka kuleta watu kwa Kristo. Nataka kufanya kitu fulani! Nataka kuzuru wagonjwa au kumfanyia Yeye kitu fulani. Ni wajibu wangu kuhubiri mazishini, ni wajibu wangu kuhubiri Injili, ni wajibu wangu kuwaombea wagonjwa. Hebu nifanye kitu kingine tena, hebu na nitoke nje na kufanya kitu kingine ambapo Mungu ataniheshimu kwacho.

¹²³ Sasa, turudie Kaini, [Nafasi tupu kwenye ukanda—Mh]. Kwa kuwa Hawa pekee ndiye aliyekuwa mwanamke aliyeumbwa na Mungu, na kama yeye hakuwa na binti ye yote wakati huyo mwanamke wa mwisho (mwanamke pekee) alipokufa, uzao wa mwanadamu ungekoma. Sivyo? Hakungekuwa tena na wanawake. Kwa hivyo ilimpasa yeye awe na binti. Na Kaini alimwoa dada yake, kwa kuwa ilimbidi afanye hivyo, hakuna mahali penginepo wanawake wanalitokea.

¹²⁴ Na ilikuwa haki na halali katika siku hizo, hata kwa Ibrahimu, na hata kwa Isaka. Isaka alimwoa binamuye. Na Ibrahimu alimwoa dada yake, dada yake hasa. Baba yake alikuwa . . . Ni mama tofauti bali baba mmoja. Na mbegu hutoka kwa mwanamume. Sara, ambaye alimzaa Isaka wa ajabu. Sivyo? Hakukuwako na watu wote duniani wakati huo.

¹²⁵ Hayo yote yalikuwa kwa mfano kuonyesha ile . . . Yako hapa, ndugu! Isaka . . . Rebeka ni mfano wa Kanisa, na Isaka ni mfano

wa Bibi-arusi, Kristo. Sivyo? Na lazima wao wawe na uhusiano wa Damu! Haleluya! Amina! Uhusiano wa Damu!

¹²⁶ Kwa hivyo Kaini alimwoa dada yake, na hilo...Ndipo walienda kule katika nchi ya Nodi. Sasa, tunaingilia somo la kilindi tukiendelea mbele kidogo, nami nafurahi haukuuliza zaidi ya hapo, (kama, “Walikuwa wapi wale wanefuli waliokuwa nchini siku hizo?” Josephus na wengineo mbali mbali wana ubishi mwingi juu ya hilo). Amina! Kama sikulipata hilo sahihi, ndugu, lirudishe tena Jumapili asubuhi. Vema.

4. Waweza kueleza Jumapili ni siku ya kwanza ya juma na Jumamosi ni siku ya saba? Wakristo huenda kanisani Jumapili, siku ya kwanza ya juma. Je, si ingaliwapasa kuenda kanisani Jumamosi, siku ya saba ya juma?

¹²⁷ Vema, sasa, rafiki mpendwa, ye yote uliyeuliza hilo, hilo ni swali nzuri sana. Ni swali la kale lililobishaniwa kati ya maelfu ya wanavyuoni siku hizi, lakini usiku huu hebu nitoe masimulizi yangu. Mwaona, hilo tu ndilo niwezalo kufanya. Kama siko sahihi, vema, ninyi—ninyi nistahimilini; na Mungu atanisamehe, mwaona, kama—kama nimekosea.

¹²⁸ Sasa, kulingana na sheria...Sasa, labda ni mtu wa Seventh-day Adventisti anayeketi hapa. Hilo lilikuwa somo langu la kwanza, lilikuwa Seventh-day Adventist. Naam. Ilikuwa Seventh-day Adventist, ndiyo niliyosoma kwanza. Nao walipokuja na kuniambia kwamba “Jumamosi ilikuwa siku ya saba,” ndugu, hiyo ilikuwa kulingana na kalenda ya Kiyahudi. Na kalenda ya Kirumi haikuimarisha, na Jumamosi hakika ikawa Jumapili. Vema, wao waliniaminisha jambo ambalo nilidhani lilikuwa sahihi. Na kwa hadiri nilivyokuwa nikisoma maandishi yao nalikuwa nikiyaamini, mia kwa mia, lakini siku moja nilishika Biblia na ndipo nikaona kwamba sivyo ilivyo. Ona?

¹²⁹ Sasa, Jumamosi ni siku ya sabato kulingana na mzunguko wa juma. Sasa, hatujui. Imegeuzwa, nasi tuna mabadiliko mengi sana huwezi kujua ilikuwa ipi. Ona? Kwa sababu sisi...Sasa, Wayahudi wanadai kuwa tuko tu karibu...hivi sasa ni karibu 1970 na kitu kulingana na mzunguko, kalenda zao. Kalenda ya Kirumi inaufanya mwaka wa 1953. Nao wana kalenda nyingine inauweka mahali pengine. Lakini hilo ndilo linalothibitisha Ukristo, yote ina msingi kule nyuma kwa kuzaliwa kwa Kristo. Mwaona, hapo ndipo tuianziapo.

¹³⁰ Sasa, lakini sasa kama siku ya saba sasa, kuna wengi sana wa watu Wapentekoste walio wa sabato—sabato washikilia sabato ambao huadhimisha sabato Jumamosi. Sasa, wao husema, “Hakuna Neno katika Biblia kwenu kuadhimisha Jumamo-... Jumapili kama siku.” Sasa nitasema jambo lile lile kuhusu sabato katika Agano Jipya. Ona? Sasa, Jumamosi ilikuwa siku ya sabato iliyopewa Wayahudi. Sasa, ilitolewa tu kwa muda.

¹³¹ Sasa huenda hili likazusha swali lingine kupinga hili. Lakini, sasa tazama. Mungu alipopumzika siku ya saba, ndipo siku ya saba haikuadhimishwa, jinsi jinsi Maandiko yanavyoagiza, kuendelea hadi karibu miaka elfu moja na mia tano. Na jangwani, Mungu aliwapa Israeli siku ya, saba kama ishara kati ya . . . Mungu.

¹³² Na Mungu alipumzika siku ya saba, siku ya ukumbusho wa mapumziko Yake. Nasema hivyo kwa manufaa ya ndugu au dada wa Seventh-day Adventist, ona, nao wana kanisa la kupendeza. Na sasa tazama, huku ni kutokubaliana kidogo juu—juu ya swali hili.

¹³³ Sasa, Mungu aliitakasa siku ya saba. Siku sita ilikuwa ni mtu. Siku ya saba ilikuwa siku ya Mungu kupumzika, ambayo ilikuwa mfano, mfano wa ule Utawala wa Miaka Elfu. Sasa, basi tazama hili, jinsi—jinsi linavyoingiana. Sasa, Yesu alipokuja duniani, kilichomsulubisha Yesu ilikuwa kwamba Yeye hakuadhimisha siku ya sabato; mashtaka mawili pekee waliyokuwa nayo dhidi ya Yesu yalikuwa kwamba “Yeye alivunja sabato, na kujifanya Mwenyewe Mungu.” Naye alisema—Yeye alikuwa Bwana wa sabato. Yeye alikuwa . . . Yeye pia alikuwa sabato ya Mungu, pia alikuwa Mungu. Kwa hivyo hawangeweza kumshtaki Yeye.

¹³⁴ Sasa, hebu niwatatuliени ninyi hili na kuwaonyesheni ni siku gani mnayepaswa kuadhimisha. Sasa, kuna Andiko? Nitauliza hili kwa manufaa yenu:

Kunalo Andiko, Ndugu Branham, linalotuambia na kutuamuru kuadhimisha Jumapili kama tu Wayahudi walivyoadhimisha Jumamosi?

¹³⁵ La, bwana, hakuna. Hakuna Andiko katika Biblia, katika Agano Jipya, kwetu sisi kuadhimisha Jumamosi wala Jumapili. Lakini kusudi la kuadhimisha Jumapili, ni ukumbusho wa kufufuka kule. Hakuna . . .

¹³⁶ Sasa, mtasema, “Katoliki ya Kirumi ilifanya hilo.” Wanadai walilifanya, lakini kama walilifanya, mtakatifu Paulo alikuwa Mkatoliki wa Kirumu, na hata Petro pia, Yohana, na Yakobo na wengineo wote, kwa kuwa wao walikutanika siku ya kwanza ya juma kwa ibada. Na, kulingana na wanahistoria, njia pekee wangetofautisha kati ya Wakristo Wayahudi na wale Wayahudi wa kiasili (wao wote walienda kwa masinagogi), lakini wengine walienda Jumamosi (waliokana kufufuka kwa Yesu), na wengine walienda Jumapili (walioamini kuwa Yesu alifufuka katika wafu). Na hiyo ilikuwa alama. Na itakuwa bado ni alama, na huenda ikaja kuwa ile chapa ya mnyama.

¹³⁷ Sasa, najua kuwa . . . Nilisikia ndugu wa Seventh-day Adventisti wadhani kwamba huo ndio muhuri wa Mungu. Wao husema, “Unatiwa muhuri kwa kuadhimisha sabato.” Hakuna Andiko katika Biblia lisemalo hayo.

138 Na hapa kuna Andiko katika Biblia lisemalo kuwa—kuwa umetiwa muhuri, Waefeso 4:30, kasema, “Wala msimhuzunishe yule Roho Mtakatifu wa Mungu; ambaye kwa yeye mliitiwa muhuri hata siku ya ukombozi,” ubatizo wa Roho Mtakatifu.

139 Sasa nitawathibitishieni kuwa muhuri wa Mungu ni ubatizo wa Roho Mtakatifu. Ona? Huo ni ubatizo wa Roho, ndio Muhuri wa Mungu. Sasa, Isaya 28, yeye alisema, “Amri juu ya amri, kanuni juu ya kanuni, huku kidogo na huku kidogo.”

140 Sasa tazama, basi, rafiki mpendwa. Sasa, watu wanaoacha kufanya kazi... Ona, watu wanajaribu kupata kitu fulani kujiokoa wenyewe. Hakuna kitu uwezacho kufanya kuhusu hilo. Unaokolewa kwa neema. Mungu hutoa wito, Mungu huokoa. Unafuata tu nya—nyayo za Mungu, hivyo tu. Huwezi kusema. Hivyo ndivyo tabia ya mwanadamu ilivyo. Wanajaribu kuacha kula nyama, wanajaribu kuadhimisha siku za sabato, wanajaribu ku... “Kama ungaliacha kufanya *hili*.” Ni... Huokolewi kwa kutokula nyama. Huokolewi kwa *hili, lile, au linginelo*. Unaokolewa kwa neema! Naye Mungu, kwa neema, hukupa Nyama, Uzima wa Milele. Mwaona ninalokusudia? Na Uzima wa Milele ni ubatizo wa Roho Mtakatifu.

141 Sasa hebu niwaonyesheni ninyi. Nini maana ya neno *sabato*? Yeyote ajuaye, inue tu mkono wako? [Dada fulani asema “Raha.”—Mh.] Raha. Hakika. *S-a-b-a-t-o*, siku ya sabato, maana yake ni “r-a-h-a,” siku ya raha. Pata somo lako lililoko kwenye kingo za karatasi katika Biblia na utazame, siku ya “Raha”. Sasa hebu tuendee, Waebrania, sura ya 4, upesi sana sasa. Nasi tuta...

142 Hili—hili ndilo swali langu la mwisho papa hapa. Na, ndugu, ona kama Ndugu Neville anayo mengine pale. Najua baadhi yao ni mafupi, kwa hivyo hatutawakawisha zaidi sana. Sasa, niradhini ninapoyachukua.

143 Sasa, unapooni neno hapa, raha, ndipo ujue maana yake ni “sabato.”

144 Sasa, hapa kuna Agano Jipya. Yesu, katika Mathayo Mt. Yeye aanzia sura ya 5 ya Mathayo Mt. naye aanza hivi: “Mmesikia wakisema, watu wa kale, ‘Usizini!’” Ati, hiyo ilikuwa nini? Torati, amri. “Lakini mimi nawaambia, kwamba, kila mtu amtazamaye mwanamke kwa kumtamani.” Akaigeuza, sivyo? “Mmesikia wakisema, wale watu wa kale, ‘Usiue’ bali mimi nawaambieni!” Aliigeuza, sivyo? (Wadhani Yeye hakugeuza torati?) Vema. Yeye alisema, “Bali mimi nawaambieni, kila mtu amwoneaye ndugu yake hasira amekwisha kuua.” Hilo halikuwepo nyuma kule katika Agano la kale, hiyo ni Agano Jipya. Yeye alipita ng’ambo yake na kuendelea zaidi ya hizo. Ona? Yeye aliendelea na kutoa amri hizo, lakini akaiacha, akairuka ile ya nne, ambayo ni siku ya saba. Sasa katika mlango wa 7 hapa...

¹⁴⁵ Katika zile Heri, haya ndiyo Yeye aliyosema alisema “Mmesikia wakisema, wale watu wa kale, ‘Usi—,’ nami nawaambieni vinginevyo. Mmesikia wakisema, ‘Jino kwa jino na jicho kwa jicho,’ lakini Mimi nawaambia! Mlisikia wakisema vinginevyo, bali Mimi nasema!”

¹⁴⁶ Sasa mwishoni mwa hayo yote, Yeye aliacha amri ya 4. Sasa, hiyo ilikuwa, “Ikumbuke siku ya sabato na kuitakasa.” Sasa Yeye alisema:

Njooni kwangu ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo; nami nitawapumzisha nafsi mweni.

¹⁴⁷ Sasa tazama, “Kila aziniye hana budi kupigwa mawe,” iliwabidi wawe katika tendo la kuzini. Sivyo? Na ilibidi ionekane ikitendwa. “Kila auaye,” ilibidi awe muuaji.

¹⁴⁸ Lakini Yesu alisema, “Kila amtazamaye mwanamke,” nafsi yake, roho, hakuna lo lote katika mwili wake sasa. Nafsi yake imekombolewa, haikuwa imekombolewa wakati huo; ilikuwa kiongozi, ona, hiyo torati. Basi, Yeye akasema, “Kila amtazamaye mwanamke kwa kumtamani amezini naye moyoni mwake.” Sasa alisema, “Mmesikia wakisema, ‘Usiue,’ bali nasema kila amwoneaye ndugu yake hasira amekwisha ua.”

¹⁴⁹ Sasa alisema, yaani, kuhusu sabato, Yeye alisema:

Njooni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo...nami nitawapumzisha nafsi zenu, sabato kwa nafsi zenu. (si ni mwili huu unaonekana, nafsi mweni.)

¹⁵⁰ Sasa, sikia—msikize Paulo sasa. Mkiweza tu... Sasa tazama, kuna joto na kila kitu, ni joto humu, pia. Lakini sasa, hebu tuchunguze hili kwa makini sasa ili tupate kulithibitisha. Sasa, Paulo, akiwaandikia Waebrania. Waebrania walikuwa akina nani? Semen. Wayahudi. Sivyo? Sasa, wao walikuwa watu wa torati, waadhimisha sabato. Sivyo, sivyo ndugu muhubiri? Walikuwa tu watu wa torati. Vema.

¹⁵¹ Sasa, Paulo anawaleta Wayahudi, kwa vivuli na mifano, akionyesha kile torati ilikuwa kwa mfano. “Torati, kwa kuwa ni kivuli cha mema yatakayokuja,” naye aendelea mbele na kuionyesha pale katika mahali fulani kama mwezi na jua. Kama mwe—mwe—mwezi ulivyo kivuli cha jua linalowaka upande ule mwingine wa nchi au sehemu nyingine ya dunia, na unarudisha tena hapa nuru. Naam, lakini sasa, na haingekuwa...lakini Waebrania 9.

¹⁵² Basi, tazama sasa katika Webrania 4, anaingilia swali la sabato. Sasa tazama:

Basi ikiwa ikaliko ahadi ya kuingia katika raha yake, na tuogope, mmoja wenu asije...

153 Sasa, Paulo akinena na watu wa sabato sasa, watu walioadhimisha siku ya sabato. “Basi na tuogope ikiwa ikaliko ahadi ya kuingia katika siku ya sabato,” kwa maneno mengine. Au kama mtachunguza maandishi yenu yaliyo ukingoni mwa kurasa, au “kuadhimisha sabato.” Ni “j” katika yangu, ya Biblia ya Scofield, au “kuadhimisha sabato.” Ona? Vema.

Basi...ikiwa ikaliko ahadi ya kuingia...asiye akaonekana ameikosa

Maana ni kweli, sisi nasi tumehubiriwa habari njema vile vile kama hao (nyuma kule chini ya torati)...Lakini neno lile lililosikiwa halikuwafaa hao. Kwa sababu halikuchanganyika na imani ndani yao waliosikia.

154 Sasa, hayo ni kule nyuma chini ya torati. Hawakuwa na imani sababu hakukuwa na msingi wa kuiwekea. Ona? Vema:

Maana sisi tulioamini tunaingia katika raha Yake; kama vile alivyosema,...

155 Sasa, raha “Yake”. Sasa, “Yake” ni Raha ya Kristo. Vema, Raha Yake, “Sabato” Yake. Na kila wakati nitatumia raha, imeandikwa pale, nitatumia “sabato,” ili mtafahamu kuhusu kuadhimisha siku fulani. Ona?

Maana sisi tulioamini tunaingia katika raha ya Sabato Yake; kama vile alivyosema,...nimeapa kwa hasira yangu,...?...hawataingia rahani mwangu; ijapokuwa...(Sasa, tazama ujumbe wa Paulo wa siku iliyotakaswa)...ijapokuwa zile kazi zilimalizika Langu kuw e kw a misingi ya ulimwengu.”

Kwa maana ameinena siku ya saba fulani kwa raha, ama sabato...(Sivyo? Nitaliweka hilo pale, ona),

Kwa maana ameinena (katika torati) siku ya saba mahali fulani hivi, Mungu alistarehe katika siku ya saba, akaziacha kazi zake zote.

156 Hiyo ilikuwa siku Yake ya saba. Sasa, Paulo angekubali kuwa Mungu aliwapa wao, hiyo ilikuwa siku ya saba. Na Mungu alistarehe siku ya saba, akaibariki siku ya sabato, akaitukuza, na akaitakasa, akifanya siku ya kustarehe. Mungu akafanya hivyo, akaacha kazi Zake zote.

Na hapa napo, Hawataingia rahani mwangu. (Yesu akinena).

157 Sasa, kuna sabato nyingine mahali fulani. Iko wapi? Sasa, kumbuka hili hapa, “Mungu alistarehe,” siku hiyo ya saba. Paulo alisema, “Walikuwa na hiyo mahali fulani,” lakini alisema, “Hawataingia rahani Mwangu,” akinena kuhusu Yesu katika Mathayo, vema.

Basi, kwa kuwa neno hili limebaki kwamba wako watu watakaolingia humo, na wale waliohubiriwa habari ile walikosa kuingia...kwa sababu ya kuasi kwao,

Aweka tena...

158 Sasa sikiza kwa makini! Kila mtu anayesikiza, aseme “Amina.” [Kusanyiko linasema “Amina! —Mh.] Sikiza:

Aweka tena siku fulani,...

159 Aweka siku hapa. Ni ipi? Kila mtu aseme mara moja. Sabato! Sivyoy? Aweka siku ya saba ya juma hapa kama sabato katika mahali hapa.

Aweka tena siku fulani, akisema katika Daudi (katika Zaburi), baada ya muda mwingi namna hii, leo; (hata Yesu alipokuja, mwaona, ule wakati wa kwanza)...ilivyonenwa, leo, kama mta...sikia sauti yake, msifanye migumu mioyo yenu. (Pale kuna raha nyingine ijayo; si ya kimwili, ya kiroho).

160 Sasa, tazama. Unasema, “Basi tuna siku ya saba, pia.” Sasa, tulia kidogo. Hebu tusome kifungu kinachofuata, ona, usiende upesi sana. Vema:

Maana kama Yesu angaliwapa...Maana kama— kama Yesu angaliwapa raha, siku ya kupumzika, asingalinena siku nyingine baadaye.

161 Yeye alipogeuza torati, toka kwa otorati hadi kwa neema, si angaliwapa siku nyingine ya raha, siku fulani ya raha, siku fulani? Lakini Yeye hakusema kamwe lo lote kuhusu sabato. Hakusema lo lote kuhusu Jumapili, hakusema lo lote kuhusu Jumamosi. Bali alisema hivi, Paulo kasema. Sasa tazama, “Pale...” Cha 19... au kifungu cha 9:

Basi imesalia sabato kwa watu wa Mungu. (Hiyo ni leo!)...Basi imesalia...sabato kwa watu wa Mungu.

Kwa maana yeye (mimi au wewe) ambaye ameingia katika raha yake (Raha ya Yesu, “Njooni kwangu ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha”), amestarehe mwenyewe katika kazi yake, kama vile Mungu alivyostarehe katika kazi zake hapo mwanzo.

162 Amina! Ndiyo hiyo sabato yako. Sivyoy?

Basi na tufanye bidii...(kasema Paulo)...kuingia katika raha ile, ili kwamba mtu ye yote asiye akaanguka kwa mfano uo huo wa kuasi (kwa siku na kwingineko, ona).

Maana neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata...kuzigawanya nafsi...

na kuyatambua...na ya...(hebu tuone)...na roho, na...(hebu kidogo)...kuzigawanya nafsi na roho, na...viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena...kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo.

Wala hakuna kiumbe...kisichokuwa wazi mbele zake, lakini vitu vyote vi utupu na kufunuliwa machoni pake yeye aliye na mambo yetu.

163 Sasa, tazama, Mungu alistarehe siku ya saba, akaiumba siku ya saba, akawapa Wayahudi kwa ajili ya ukumbusho. Ninanena kuhusu Mtakatifu Paulo sasa, ona. Isikie! Sasa, mwadhani yeye alikuwa akiileta? Je, wadhani angekuwa na haki? Sasa, yeye alisemaje katika Wagalatia 1:8? “Lakini ijapokuwa malaika wa Mbinguni atawahubiri ninyi Injili yo yote isipokuwa hiyo tuliyowahubiri, na alaaniwe.” Ona, injili ni dhahiri. Sasa, tazama.

164 “Vema Ndugu Branham, sasa nifanyeje, nimwamini Yesu Kristo tu?” La. Hiyo siyo Raha.

165 Sasa, ukitaka kujua...Wangapi wangependa kujua Raha ya Wakristo ni nini, semeni “Amina.” [Kusanyiko lasema, “Amina! —Mh.] Sasa, mwaweza kuiweka alama mkipenda, Isaya 28. Yeye alisema “Amri juu ya amri—amri,” akinena. “Amri juu ya amri, kanuni juu ya kanuni, huku kidogo na huku kidogo, na shikilia sana yale yaliyo mema.” Nabii yule akinena kuhusu wakati unaokuja, kuhusu Raha, sabato. Soma hiyo sura yote, ona, yeye anasema, “Nyakati zile siku ya sabato itakapo—itakapoondolewa,” nao watauza viatu Jumamosi kama tu vile walivyofanya Jumatatu, na kadhalika. Mwaona? Kasema, “Ishara hii itakuwepo lini?” Kasema:

...amri juu ya amri...kanuni juu ya kanuni; huku kidogo, na huku kidogo: shikilia sana yale yaliyo mema.

La, bali kwa midomo ya watu wageni, na kwa lugha nyingine nitasema na watu hawa;

...Hii ndiyo sabato, ile raha ambayo nilisema wapaswa waingie. Bali kwa haya yote walifanya mioyo yao migumu na kutikisa vichwa vyao kuikataa. (Jambo lile lile tu walilofanya siku ya Pentekoste Roho Mtakatifu aliposhuka juu ya watu, na Roho Mtakatifu alipotolewa kwa watu mara ya kwanza nyuma kule katika siku ya Pentekoste. Hiyo ndiyo Raha, sabato kwa watu wa Mungu)...

166 Kwa hivyo sababu pekee tuadhimishayo Jumapili, ilianzishwa na baba zetu wa Biblia, Mtakatifu Paulo, Yohana, Mathayo, Marko, Luka na wengineo wote, walienda nyuma kwa nyumba, walipokea ushirika siku ya kwanza ya juma mitume walipokusanyika, na iliitwa, si sabato, bali siku ya Bwana.

¹⁶⁷ Yohana alisema, kwenye kile kisiwa cha Patmo, tayari kulikuwa maadhimisho ya sabato kanisani, “Nalikuwa katika Roho siku ya Bwana.” Naam, Ona? Na ndipo yeye aliona . . .

¹⁶⁸ Na—na, sasa, siku ya Bwana ni—ni ile siku Bwana aliyofufuka. Naam, enda upate wanahistoria, Josephus, Actibus [Hatuna hakika ya herufi—Mh.], wengineo wengi. Ama si Actibus, ee, siwezi . . . Mmoja wa hao waandishi wa mashariki, na utatambua nyuma pale. Wanahistoria wa kanisa, *Kitabu cha Wafia Imani cha Fox*, wengineo wengi, na utatambua kuwa tofauti pekee . . . Wao ni kundi la Wayahudi. Mmoja wao aliwaita “wala watu,” hao walikuwa Wakristo. Wao walisema, “Kuna mtu aliyeuawa na Pontio Pilato na wanafunzi wakaja na kuiba mwili wake. Nao wakauficha, na kila—kila Jumapili wao huenda kula sehemu yake.” Walikuwa wakifanya ushirika, mwaona. Wao tu . . . Wao walikuwa wakila mwili Wake, mwaona. Wao walisema walikuwa wakila mwili wa Bwana, ushirika. Nao hawakujua ilikuwa ni nini, naye alisema, “Walikuwa wala watu.” Kasema, “Wao huenda kuula kwenye siku ya kwanza ya juma, wao hukutanika pamoja na kula mwili wa mtu huyu.”

¹⁶⁹ Na njia pekee ambayo ungetambua kama walikuwa waadhimisha sabato na hukanusha kabisa ufufuo, au kama walikuwa Wakristo na walamini ufufuo, wengine walienda kanisani Jumamosi na wengine walienda kanisani Jumapili, ambayo ilikuwa alama kati yao.

¹⁷⁰ Hilo ni nzito, sivyo? Vema. Natumaini limejibiwa. Roho Mtakatifu ni . . .

¹⁷¹ Sasa, una kitu fulani pale, ndugu? Unataka . . . Je, unataka—unataka kuja na kulijibu? Hebu tuone, papa hapa. Ee, naam.

5. Je, Wayahudi watakuwa na nafasi kuokoka baada ya muda wa wakati wa Mataifa kwisha?

¹⁷² Ee, lo, kama hilo si nzuri! Enhee, hatuna wakati wa kuliendea vizuri sana, lakini hebu niwaambieni hili. Nisadikini, nitawaonyesheni ninyi. Kwa . . . Kama mtanisadiki, kama nilivyoeleza kwa Mungu, basi nendeni mkaichunguze, ona, na ndipo mtatambua. Kwa sababu nakisia . . . Siwezi kuona saa ya ukutani, bali nakisia kuwa umepita . . . Ni saa ngapi? Ati nini? Saa tatu na nusu. Ningali naenda hospitalini, na pia nitaenda New Albany, niondoke Jeff. saa tisa na dakika ishirini na tano usiku. Kwa hivyo . . . Nami sijapata kwenda kitandani kabla ya saa nane au saa tisa usiku usiku wo wote juma hili.

¹⁷³ Sasa tazama hapa, upesi sasa, kupata hili. Naam, rafiki yangu mpendwa Mkristo, siku za Mataifa zimekwisha, zimekwisha, zinakwisha hivi sasa. Na Mungu atarudi kwa Wayahudi. Na hebu niliambie kania hili ndogo ninaloombea mara kwa mara. Na unabii toka mahali mbalimbali nchini unamiminika ndani humu kuhusu hili. Naamini kuwa

Wayahudi...Sasa, vaeni makoti yenu kwa dakika moja hivi, sasa.

174 Wayahudi hawajawahi kufahamu hili jambo moja la kanisa la Kikristo. Wayahudi wameniambia mara nyingi. “Ndugu, huwezi kumkata Mungu katika vipande vitatu na ukanipa.” Wayahudi wana Mungu mmoja, na huyo ni Yehova.

175 Na Mataifa hawakufahamu kweli hiyo; zaidi sana hata ni kama wamenaswa, bado, kwa maarifa. Naamini yeye—yeye ana—anafahamu, kwamba hakuna miungu mitatu. Kuna Mungu mmoja, dhihirisho tatu. Utu utatu katika Nafsi moja. Na unapoweza kufahamu ujumbe huu, niliongea na Hyman Appleman...Wengi wenu mnamjua. Yeye alisema, “Ndugu Branham, ukipeleka ujumbe huo kule Palestina pamoja na ishara na maajabu,” kasema, “kutakuwa na Wayahudi milioni watakaompokea Yesu Kristo kama Mwokozi wao.” Ona naam. Basi, nilisema...

176 Ujumbe tulio nao hapa ni huu. Yesu alikuwa Yehova aliyejificha katika mwili, akashuka chini ali amejificha. Sasa Mungu (Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu) si kama kidole chako, kimoja, kama watu fulani wadhanivyo. Yote ni kama tu...La, Mungu ni...Niliwawaonyesha tu muda mchache uliopita, ona, kuwa kuna utatu katika yule Mmoja.

177 Mimi ni utatu katika mmoja. Mimi ni nafsi, mwili na roho katika mtu mmoja. Sivyo? Hakika. Mimi—mimi nimefanywa kwa—kwa chembechembe hai, damu, na mishipa ya fahamu, na hali ni kiumbe kimoja. Ona? Kila kitu unachokitazama kiko katika utatu, na utatu katika mmoja.

178 Kulikuwako utatu katika safina. Sakafu ya chini, vile vitu vitambaavyo; orofa ya pili kwa ajili ya ndege, vitu vipurukavyo; na orofa ya tatu kwa ajili ya Nuhu na jamaa yake. Kila kitu!

179 Katika ile hema. Kulikuwako na makutano, mahali patakatifu, mahali Patakatifu pa patakatifu. Ona?

180 Na kumekuwa na muda mtatu wa wakati. Ule wa Ubaba, ule wa Uwana, na ule wa Roho Mtakatifu. Mwaona ninalokusudia? Lakini hao watatu wote ni...Hatusemi, “Miungu yetu.” Huo ni ukafiri, na wayahudi wajua hilo. Lakini unapoweza kuwahakikishia kuwa huyu Yesu ni Mungu, Yehova Mungu, si nafsi ya pili, wala nafsi ya tatu, ni Nafsi moja ile ile wakati wote akijidhihisha Mwenyewe. Ona? Na ndipo pamoja na ishara na maajabu kuthibitisha kuwa amefufuka toka kwa wafu.

181 Na huyu Daktari Reedhead...

182 Ndugu nyuma kule, mwalimu hapa kanisani...mwalimu pale...mwalimu wa shule, hapa kanisani. Nami nilimwuliza... Nami nilisalimiana na mke wake na kitoto chake nyuma kule. Yeye alikuwa nje pale kunisikia nikihubiri hivi majuzi, nafikiri wao wako humu, iwapo hawajaondoka, naamini yeye ni

mwalimu wa shule katika Louisville. Haidhuru, walikuwa nje pale kumsikia.

183 Ni jambo lisilosahaulika, mtu yule alikuja nyumbani kwangu, yeye na mwingine (na Myahudi fulani), miezi michache iliyopita. Naye alisema, “Ndugu Branham, nina shahada za chuoni *nyingi sana* katika Bob Jones. Nime... toka Wheaton.” Elimu yote ambayo ingeweza kurundikwa ndani yake! Kasema, “Nimemwamini Mungu tangu nilipokuwa mtoto mdogo. Kisha kasema, “Bado maisha yangu yana utupu!” Yeye kasema, “Je, waalimu wale wamekosea?”

184 Wazo lake ndilo hili. Kama ye yote... Kama baadhi yenu mlikuwa kwa Mlango Uliofunguliwa usiku uliopita, walipokuwa waki—wakihubiri, pamoja. Yeye alisema, “Nilipopata vyangu...” Sasa, sikizeni, maskani madogo, kwa maombi yenu na vitu vilivyonisaidia, sikizeni, maskani madogo, kwa maombi yenu hapa nyumbani.

185 Yeye alikuja nyumbani kwangu, naye kasema, “Ndugu Branham,” kasema, “Nimeshikwa na bumbuwazi.” Yeye akasema, “Kuna kitu kinachopita yale nimeamini na kukubali, Kristo kama Mwokozi wangu? Nami naamini kuwa nimezaliwa mara ya pili kwa Roho, lakini sina ushuhuda wa lo lote.”

186 Nilisema, “Ndugu, nachukia kusema hivyo, bali waalimu wako wamekudanganya wewe, shule zako.”

187 Tazama, kama ni—niwezavyo kusema hilo, siamini kubebwa-bebwa hata Mbinguni, “Je, mnaamini hili makanisani mwenu?” Sikuwahi jua lo lote bali yale...” Biblia yasema hili, waamini hilo?” Shetani anaamini na kutenemeka! Si kile unachoamini. Roho yako inapaswa ishuhudia na Roho Wake kuwa ninyi mu wana na binti za Mungu, kwa kuzaliwa mara ya pili na kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu.

188 Yeye alisema, “Ndugu Branham, waonaje kuhusu Wapentekoste?”

189 Nami nilisema, “Hiyo ndiyo sababu nawashughulikia wao. Hiyo ndiyo sababu ni—nawahangaikia, wana kitu fulani msicho nacho.” Nilisema, “Ingawa wana uzushi wao na kila kitu, wana kweli fulani msiyojua lo lote kuihusu.” Nami nilikuwa nikiongea na mmoja wa watu wakuu sana Amerika, papo hapo. Naam, bwana. Yeye ni rais wa Sudan Missions, ndiyo kubwa sana ulimwenguni kote, ya kidesturi kupindukia. Yeye alijua Maandiko, na *kufa, kuzikwa na kufufuka*, anavihubiri tu kama nyumba inayoteketea. Lakini hiyo siyo. Shetani aweza kufanya hivyo, pai. Shetani ni wa kiasili kama tu awezavyo kuwa.

190 Lakini, ndugu, Yesu Kristo alisema, “Mtu asipozaliwa kwa Roho wa Mungu hataona Ufalme wa Mungu.”

191 Si kwa sababu tu wasema, “Naam, naamini hilo. Naam, ni—ninaamini hiyo ndiyo njia. Naamini hilo. Naam.” Hilo halifai

kitu. Yabidi uwe ujuzi hasa wa kuzaliwa mara ya pili. Yapasa iwe kitu fulani kati yako na Mungu hata ujue umepita toka mautini kuingia Uzamani.

¹⁹² Kasema, “Ndugu Branham, ningeweza kumpokea Roho Mtakatifu?”

¹⁹³ Nilisema, “Niliweka tu mikono kwa Hyman Appleman chini pale, naye akapokea ubatizo wa Roho Mtakatifu.”

¹⁹⁴ Huyu Myahudi mwingine akaanza kulia, na akavunja bilauri kwenye ile meza ya kahawa pale, machozi yakajaa pale. Wote wawili walisema, “Ndugu Branham, tunampokeaje Roho Mtakatifu?” Wanavyuoni! Werevu sana, wenye kisomo! Watu bora sana walioko nchini!

¹⁹⁵ Nami nilisema, “Njia ya kimitume ya kumpokea Roho Mtakatifu ni kwa kuweka mikono juu yao.” Naam.

¹⁹⁶ “Kuwarekea mikono.” Anania alikuja kumwekea Paulo mikono ili yeye apokee kuona kwake na ajazwe na Roho Mtakatifu.

¹⁹⁷ Filipo alienda chini kule na kuhubiri chini kule, na kubatiza kundi lote chini kule katika Jina la Yesu Kristo. Roho Mtakatifu hakuwa amemshukia ye yote, kwa sababu Petro ndiye aliyekuwa na zile funguo, Naye akaja kule, na kuweka mikono yake juu yao, nao wakampokea Roho Mtakatifu. Sivyoye?

¹⁹⁸ Paulo, katika Matendo 19, baada ya kupitia pande za juu. Apolo, alikuwa mfano wa Billy Granham juu pale, alikuwa na mkutano wa ufufuo mkubwa na wakati wa kuchangamsha. Yeye akawauliza, “Je, mmpokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?” Hilo kundi la Wabaptisti.

¹⁹⁹ Wao walisema, “Sisi ni wafuasi wa Yohana. Twajua! Apolo ndiye mhubiri wetu, yeye ni mwana-sheria aliyelongoka, mtu mwerevu mno nchini.”

²⁰⁰ Yeye alisema, “Lakini je, Mmpokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?”

Yeye akasema, “Hatukujua kama kuna Roho Mtakatifu.”

Kasema, “Basi mlibatizwaje?”

Kasema, “Tulibatizwa kwa ubatizo wa Yohana.”

²⁰¹ Kasema, “Yeye alibatiza kwa toba, akisema kwamba mumwamini Yeye ajaye, Yesu Kristo.” Na waliposikia Hayo, wakabatizwa katika Jina la Yesu Kristo. Na Paulo akawawekea mikono yake juu yao nao wakapokea Roho Mtakatifu, wakaanza kunena kwa lugha na kumtukuza Mungu. Hayo ni wazi tu kama ni juavyo Maandiko.

²⁰² Sasa, tazama, rafiki! Huenda kukawa na tofauti ndogo hapa kwa maoni yako, kwa sababu umetatanishwa katika kila kitu. Lakini hebu tulifafanue, usijaribu kuweka tafsiri yako. Sema yale Biblia isemayo, yaache tu hivi.

203 Nami nilisema, “Jambo pekee nijualo, ndugu, ni kuwekea mikono juu yao wale wanaotafuta Roho Mtakatifu.”

204 Yeye alisema, “Je, waweza kutuwekea mikono na—na kumwomba Mungu atubariki na atupe Roho Mtakatifu?”

205 Nilisema, “Nitafanya hivyo.” Nasi tulipiga magoti sakafuni, nami nikaomba na kuwawekea mikono. Na majuma machache baadaye wote wawili wakampokea Roho Mtakatifu. Na huyu Daktari Reedhead alimpokea Roho Mtakatifu, akanena kwa lugha. Naam, bwana.

206 Na Sudan Missions yenu ikasema, “Hatuna nafasi kwa mtu anayenena kwa lugha.”

207 Naye alinijia na kusema, “Mtu anayenena kwa lugha?”

208 “Mbona, mbona,” nilisema, “Hawana nafasi kwa Yesu Kristo, maana Yesu Kristo alinena kwa lugha, na akafa, akinena kwa lugha zisizojulikana.”

209 Hawangeweza kukubali mafundisho ya Paulo, Paulo alinena kwa lugha zaidi ya wao wote.

210 Mmoja aliniambia jana, kasema, “Heri ninene maneno matano kwa akili zangu.”

211 Lakini mafundisho ya Paulo yalisema, “Takeni sana kuhutubu, wala msizuie kunena kwa lugha.” Nao wanazuiwa kunena kwa lugha!

212 Kunena kwa lugha ni karama ya Kiungu ya Mungu ambayo ni mali ya kanisa vivyo hivyo leo kama ilivyokuwa hapo mwanzo. Ni Kweli hasa. Naam, kabisa! Hilo ni fundisho la Biblia. Ni karama ya Kiungu, nanyi mwakana hilo jinsi m—mkanavyo kule kuzaliwa mara ya pili, mnakana kila kitu ambacho Yesu alifundisha mnapojaribu kukatilia hilo mbali.

213 Sasa, waweza kuenda upande kwa hilo, wengi wao wamefanya hivyo. Lakini ninasema, “Hilo lina mahali pake.” Ni kama tu viatu; unaponunua viatu, ndimi zimo humo ndani. Naam. Unapokuwa katika Mwili wa Kristo, Mungu ameandaa meza yote. Ndugu, yeye ana upendo, ana furaha.

214 Kama nilienda mezani kwako na kuketi pale, nawe ukasema, “Mhubiri karibu ule pamoja nami,” naamini unanipenda. Na una maharagwe na viazi na karati na kuku iliyokaangwa na sambusa ya boga na maziwa ya mtindi, kila kitu kimewekwa pale. Basi, naamini ningekaribishwa tu viazi jinsi ningalikaribishwa maharagwe. Jambo ni kwamba, naamini ningekaribishwa kuku kama nilivyokaribishwa sambusa. Vyote viko mezani. Na kitu pekee kinipasacho kufanya ni kusema, “Waweza nisogezea sambusa tafadhali?” Nami naamini kwa moyo mzuri na mkunjufu, upendo wako kwangu, ungesema, “Naam, ndugu yangu, chakua kipande kikubwa kitamu.” Sivyo? Kama ningesema, “Tafadhali nisogezee viazi?” “Naam, hakika, ndugu yangu, hivi hapa”

215 Na kila baraka ya ukombozi ambayo Yesu Kristo aliifia na kuinunua katika utakaso Wake Kalvari, iko mezani na kila mwamini anaketi mbele yake. Haleluya! Kama nahitaji uponyaji, nitasema, “Baba, nisogezee uponyaji,” nami naumwaga kwenye sahani yangu na kula kikubwa... Naam, ukitaka kufa kwa njaa, endelea. Naam, bwana. Na unabii, kunena kwa lugha... .

216 Na—na ndipo mtu fulani aliandika ndani mle, yeye hakujua kuwa nilinena... Mimi mwenyewe nilikuwa nimenena kwa lugha. Naye alikuwa akiandika hiki kitabu, utakipata kimesambazwa duniani mwote. Na mbali na hilo, mtu huyu ana wahudumu maarufu ishirini na watano wa chuo cha Biblia cha Moody wanaotafuta karama ya kunena kwa lugha. Watu wa kiasili wamepinduliwa. *Maisha ya Kikristo*, mwezi huu—huu, tazama gazeti la *Maisha ya Kikristo* la mwezi huu, kurasa ya kumi na tisa, na mtazame huyo daktari mkuu wa theologia, akisema, “Je, tutakubali hili? Je, tumepoteza kitu fulani?”

217 Nasikia mvua nyingi ikija! Kunao watu wanaokata kona, lakini imefikia mahali ambapo Mungu anautikisa ulimwengu wa Mataifa kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, akiwamiminia utimilifu wote na nguvu na ishara na maajabu. Sababu nashikilia... Wapentekoste wamesukumwa pembeni na kukosea katika mambo mbali mbali kama hayo, wakati ulikuwa haujafika bado. Hiyo ndiyo sababu wamekuwa na ushupavu huu wote wa dini. Lakini hiyo ni ahadi ya Kiungu ya Mungu na Neno la Kiungu la Mungu, na sharti itimie kwa kuwa Mungu amesema hivyo. Nami naamini kwamba kabla muda wa wakati wa Mataifa haujakwisha, Mungu atawamwagia wa kiasili.

218 Mwaweza kuyasoma katika *Reader's Digest* mwezi huu, hili toleo la Agosti. Endeni mkasome, jinsi huyo mhubiri Mmethodisti chini pale mimbarani mle, alimwomba mtu aliyelala hospitalini akifa, na ushuhuda wa Roho Mtakatifu ukaja na mtu huyo akaponywa papo hapo Haleluiya! Hakika. Mungu yuna uponyaji wa Kiungu mezani hapa! Yeye ana unabii mezani hapa! Ana kunena kwa lugha mezani hapa! Ana karama tisa za kiroho katika Mwili huo, na umekaribishwa kwa kila moja wazo! Haleluya! Naam, bwana, ndizo hizi hapa.

Je, . . . Mwishoni mwa Mataifa, je, Wayahudi watarudishwa?

219 Naam, bwana. Maandiko mengi, dada, ndugu, ye yote yule, Yoeli kwa mfano, “Yaliyosazwa na parare yameliwa na tunutu,” na kadhalika, mti huo. Na Yesu alisema Mwenyewe jinsi wangefukuzwa na kadhalika. Ee, Maandiko yote, Danieli na kila mahali, yananena hayo. Naam, Yesu alisema, “Mwonapo mtini ukiisha kuchipuka majani, tambueni ya kuwa wakati u karibu.”

Naamini hili lingine linashughulikia jambo lilo hilo.

6. Je, waamini kuwa kurudi kwa Wayahudi—Wayahudi Palestina ni utimizo wa unabii wa Biblia? Tulisikia unaenda Palestina, hilo ni kweli?

²²⁰ Naam. Naam, bwana. Hebu niwaambie jambo fulani, mojawapo kuu zaidi. . . Mkitaka kuona ni wakati gani mwakani, mnatazama kalenda. Mkitaka kuona ni saa ngani za usiku, mnatazama saa. Mkitaka kuona ni siku gani mnayoishi, tazameni Wayahudi walipo. Hao ndio saa ya Mungu.

²²¹ Na tazama! Usiku ule ule, siku ile ile, ambayo yule malaika wa Bwana alikutana nami, 1946, Mei tarehe saba, kule Green's Mill, Indiana, siku iyo hiyo mkataba wa amani ulitiwa sahihi kwa ajili ya Wayahudi nao wakawa taifa thabiti kwa mara ya kwanza kwa miaka elfu mbili na mia tano. Haleluya!

²²² Na, usiku huu, ile bendera ya zamani sana ulimwenguni, ile nyota yenye pembe sita ya Daudi, inapepea Yerusalemu kwa mara ya kwanza katika miaka elfu mbili na mia tano, tangu uhamisho wa Babeli. Yesu alisema, "Mwonapo mtini ukiisha kuchipuka." Ndilo hilo! Pale Yeye alisema, "Jifunzeni mfano. Mwasema, 'majira ya kiangazi yamekaribia.' Mwonapo hili, jueni wakati u karibu." Tuko katika wakati wa mwisho kabisa.

²²³ Tazama jinsi lile "chukizo" la Danieli, na kadhalika, mwajua, Yesu aliposema. "Yule Mtawala mkuu ajapo, Yeye atatoa unabii siku elfu moja na mia mbili na sitini," ambazo zilikuwa miaka mitatu na miezi sita. Na hizo ndizo hasa Yesu alihubiri. Yeye aliwajia Wayahudi pekee, ndipo Yeye atakatiliwa mbali kama dhabihu kwa—kwa ajili ya watu. "Na lile chukizo la uharibifu," Waislamu walijenga ule Uislamu wa Omar pale. "Nao wangekanyaga kuta za Yerusalemu mpaka" (whiu! mpaka lini?) "majira ya Mataifa yakapotimia." Na ndipo Yeye atawarudia Wayahudi tena, na hapo ndipo vile vita vya Amagedoni vitakapopiganwa. . . Hapo Yeye aliwaita Mataifa, awachukue watu kwa ajili ya Jina Lake, Bibi-arusi Wake. Tazama. Naam, bwana. Wale mia na arobaini na nne elfu wote ni Wayahudi waliokombolewa ambao wangali watasimama pale. Haya yote. . .

²²⁴ Kisha Kanisa linyakuliwapo, Musa na Eliya wataonekana, katika Ufunuo 11, nao watahubiri Yesu Kristo kwao. Na Roho Mtakatifu anatwaliwa toka kwa Mataifa, na kunyakuliwa kwaja kusudi Kanisa lipate kutwaliwa. Na Wayahudi waliobaki hapa itahubiriwa kwao kwa miaka mitatu na nusu kwa sababu yeye alisema, "Muda wa majuma sabini umeamriwa juu ya watu wako, na Masihi atakatiliwa kati ya majuma hayo." Yeye alipokuwa akiondoshwa, Mataifa walipewa nafasi na wao wana miaka mitatu na nusu watakayohubiri kwao, kuhusu Yesu Kristo.

225 Hakika, Wayahudi wanakuja. Nami naamini, ndugu, kuwa tufikapo kule Palestina wakati huu... Ee, omba! Wanasoma Biblia hiyo.

226 Tamshi moja tu zaidi, ndipo nina swali moja fupi ndogo hapa, na ni hayo tu. Hii hapa nadhani ni ombi.

227 Tazama hili! Daktari Reedhead kasema, huku amesimama pale akiongea na Mwislamu mwerevu...

228 Sasa, tegeeni masikio yenu kwa makini sana. Mwislamu, nilikuwa nao wapatao elfu ishirini wakimjia Bwana Yesu walipoona ishara na maajabu kule Afrika. Walikuwa karibu elfu ishirini, jumla ya watu elfu thelathini; nadhani waliomjia walikuwa elfu kumi, kwa sababu wengi wao walikuwa—walikuwa Waislamu. Na waliposimama pale, nami nikasema, “Nani kati ya manabii wenu hekaluni awezaye kumponya mtu huyu?” Nilisema, “ipi ya sanamu zenu, ninyi wenyeji, yaweza kumponya mtu huyu?” Nilisema, “Hakuna hata mmoja wao! Hamna nabii hekaluni... samahani, hamna kasisi.” Nami nilisema, “Hakuna sanamu zingelifanya hayo. Wala mimi pia. Bali Mungu aliye Mbinguni alimwinua Mwanawe Yesu Kristo aliye miongoni mwa watu leo, aliyemponya kabisa kama mumwonavyo sasa amesimama.” Mtu aliyekuwa na mnyororo shingoni mwake, ilibidi wamwongoze kama mbwa. Mara akasimama kwa miguu yake, ameponywa na yu mzima.

229 Na Daktari Reedhead aliniambia usiku uliopita tulipokuwa tumeketi kwenye motokaa, alisema, “Ee, lo!” akiwaza hilo. Yeye alimwambia huyu Mwislamu aliyemjia, na kusema yeye alikuwa akiongea na Mwislamu huyu, mtu aliyeelimika sana. Yeye kasema, “Vema, bwana, mbona usimkane maskini nabii wako aliyekufa, Mohammed?”

230 Sasa, kumbuka, Waislamu wanamwamini Mungu. Kule katika—katika Afrika, “ngoma” kubwa, huning’inizwa hivyo. Nao huchukua nyundo kubwa ya mpira na kuigonga hivyo, na inalia nchini kote. Na kila Mwislamu husimama, na makasisi hutembea hadi waliko watu, na kusema, “Kuna Mungu mmoja tu na wa kweli, aishiye, na Mohammed ndiye nabii Wake.”

231 Hao ni wana wa Ishimaeli. Ona, Hajiri, hao ni wana wa Ibrahimu kwa Hajiri. Ona? Wanamwamini Yehova Mungu wa kweli, lakini wao hudhani Yesu... (Aliyekuwa... Yeye ni Mkombozi *wetu*, aliyetumwa kwa Mataifa toka kwa mwanamke muungwana; Isaka, ona, na kupitia kwa Sara). Na sasa, wao walipitia kwa Hajiri, Ishimaeli, na kukatokea Waislamu.

232 Na pale kaburini mwa Mohammed, yapasa uende utazeme, ni la kuvutia, lile kaburi kubwa pale. Na kwa miaka elfu mbili kumekuwa na farasi mweupe aliye na tandiko, amesimama pale. Mohammed aliahidi kwamba angefufuka toka kwa wafu siku moja na aruke juu ya farasi huyo na kuuteka ulimwengu. Na kila—kila baada ya muda fulani wao hubadili farasi mmoja

kwa mwignine; akingojea pale pamoja na mlinzi mwaminifu, amesimama, akingoja Mohammed afufuke toka kwa wafu. Miaka elfu mbili imepita tangu wakati huo.

²³³ Wanaamini Yesu, wao husema kwamba Yeye alikuwa nabii. Kwenye zile kuta za Yerusalemu kuna jengo kubwa takatifu lililojengwa, ambamo Mohammed atakuja kukaa. Na jengo ndogo mle chini, ambalo ni la Yesu. Ona, walisema, “Yesu hakusulubiwa, wana changanikiwa na hilo.” Kasema, “Yeye alipanda farasi akaenda zake.” Ona? Sasa, wao—wao wanaamini hilo.

²³⁴ Wanaweka tone nyekundu kati ya macho yao. Watu wale wanaokwenda India, mtaliona. Lo, watasimama pale kwa maelfu.

²³⁵ Na ndipo Daktari Reedhead alisema alikuwa amesimama pale, naye alisema, “Sasa, mbona msikane maskini nabii huyo mfu mkampokee Yeye Yule aliyefufuka toka kwa wafu, Kristo aishiye?” Sasa, yeye alikuwa mwerevu sana naye alijua jinsi ya kutamka maneno yake.

²³⁶ Kasema yule Mwislamu alimtazama, (mwerevu, mtu aliyesoma sana, papa hapa Amerika, aliyesomea hapa) yeye kasema, “Bwana, kwa hisani yako, bwana, Yesu wako aliyefufuka aweza kunitendea nini kuliko yale nabii wangu mfu amenitendea?” Kasema, “Nabii wangu mfu aliniahidi Uzima baada ya mauti. Hilo ndilo Yesu wako alifanya.” Vema, kweli. Kasema, “Sasa, wote wawili waliandika kitabu. Unakiamini kilichoandikwa na Yesu, naamini kilichoandikwa na Mohammed. Wote wawili wanaahidi Uzima.” Kasema, “Yesu wako aweza kunitendea mimi nini kuliko Mohammed wa—wangu awezavyo?” Vema, huyo mtu, bila shaka, alisema kweli. Yeye alisema, “Hebu kidogo tu, bwana, kwa hisani yako!” Yeye alisema, “Mohammed wangu hakuniahidi vitu kama Yesu wako alivyofanya. Yesu wako aliahidi... Wao walisema, ‘Yeye alifufuka’ naye angekuwa nawe wakati wote, hata ukamilifu wa dahari; na ishara na maaajabu ambayo alifanya nanyi mngefanya pia, hata ukamilifu wa dahari. Mngewaponya wagonjwa, na kufufua wafu, na kuwatakasa wenye ukoma, na kutoa pepo.” Kasema, “Nilisomea Ukristo, vilivyo.” Kasema, “Sasa hebu nione ninyi walimu mkimdhahirisha Yesu Kristo, nami nitaamini Yeye alifufuka katika wafu. Lakini, nje ya hayo... Mohammed hakutuahidi vitu kama hivyo, yeye alituahidi tu Uzima baada ya mauti. Nanyi hufunza jambo lile lile, na kuepa mengine.” Mtu huyo alikuwa sahihi, yule Mwislamu alisema kweli hasa.

²³⁷ Daktari Reedhead alisema alisimama na kulia. Kasema, “Ndugu Branham, niliwaza juu yako.” Naye akaja upesi hapa, na kuingia ndani mle, nami nikamwekea mikono yangu juu yake, na ubatizo wa Roho Mtakatifu ukamjia. Na sasa hata yeye huona

maono na kadhalika. Sasa hebu na yule Mwislamu akutane naye! Yeye ni mtu tofauti!

²³⁸ Nasema Yesu wetu aliyefufuka katika wafu, Yeye yuaishi leo. Naye yuatenda mambo yale yale leo aliyoyatenda wakati huo, aina zote za ishara na maajabu. Nanyi watu kiasili mnaoketi hapa mkijaribu kuyakana, na kukosa ile sehemu iliyo muhimu ya Biblia. Naam hasa. Yesu Kristo, yule Mwana wa Mungu aliyefufuka, aweza kunena kwa lugha kupitia kwako, Yeye aweza kutabiri kupitia kwako, aweza kuona maono kupitia kwako, aweza kutafsiri lugha zisizojulikana kupitia kwako. Na hivyo vyote ni sehemu Yake.

²³⁹ Na kuchukua hii sehemu Yake na kuacha sehemu *ile* Yake, ingekuwa kama kunikata mimi katika vipande viwili na kuchukua tangu paja na mguu kurudi chini na kusema umenipata, hali sehemu *hii* hauwezi kuipokea.

²⁴⁰ Yakupasa unipokee mimi kabisa... Na hiyo ndiyo sababu Mimi ni mhubiri wa Injili nzima anayeamini kuwa kila alichosema Mungu ni Kweli. Amina! Utukufu! Najisikia kama mtakatifu anayejigaragaza sasa hivi. Naam, bwana. Naamini hilo!

7. Mathayo 24:29, yanena kuhusu “Jua litatiwa giza, na mwezi hautatoa mwanga wake, na nyota zitaanguka toka mbinguni.” Je, hili litatendeka kabla au baada ya Kunyakuliwa, au kabla tu ya Yesu kuja...kutawala dunia?

²⁴¹ Ninavyoamini mimi, sasa, singe...Sijui, nadhani yeye ananena kuhusu Mathayo 24, pale. Sasa Yesu ananena kuhusu nyota na vinginevyo kuanguka, naamini hiyo ni kabla ya ule wakati wa Dhiki kuu kuingia duniani.

²⁴² Sasa, nilikuwa na wazo la ajabu sana hapa ambalo wengi wenu hamtakubaliana nami, maana nadhani baadhi yenu watu wa kale mlisikia mafundisho tuliyofundisha. Ona, siamini Kanisa litapitia katika ule wakati wa ile Dhiki. Naamini Kanisa lita...Tazama, Mimi...Njinsi pekee ambayo Mimi hufundisha agano Jipya ni kwa vivuli vya Agano la Kale tu, kama tu vile Roho Mtakatifu hapa alivyo siku ya sabato na mengineyo. Kila kitu ni kivuli nyuma kule.

²⁴³ Sasa, tazama nyuma katika Agano la Kale. Uonapo mapigo yakianguka, walikuwa kule Misri. Sivyo? Na Mungu alikuwa akiwaondoa watu waende kwenye nchi ya ahadi. Sivyo? Na Israeli haikupokea pigo hata moja. Kama tu vile mapigo hayo...kabla hayajatukia, walienda Gosheni. Sivyo? Na—jua halikuzimika, hakuna mbu waliokuja, hakuna vyura waliokuwepo pale, wala chawa kule, wala dhoruba haikuwepo kule, hamna umeme kule, wala kuuawa kwa ng’ombe, na kila kitu walichokuwa nacho kilihifadhiwa Gosheni. Sivyo? Ni mfano wa Kanisa kuondoka kabla ya ule wakati wa ile Dhiki iliyo

kuu. Yesu alisema, “Mambo haya yaanzapo kutokea, mkaviinue vichwa vyenu, ukombozi wenu umekaribia.” Ona?

244 Naamini kuwa mwezi na jua na nyota...Ndipo wao walisema kuwa...Nitaisoma haidhuru, kasema, “Watu wakakimbia na kujificha. Nao...na kuangukia...wakajaribu kujiua, na wakashindwa, na kadhalika.” Naamini hilo litatendeka kabla tu ya ile Dhiki.

245 Sasa, tazama, ile Dhiki ijapo. Ile Dhiki ianzapo, Kanisa litanyakuliwa. Sasa, kumbuka, ni kanisa tu la kawaida lisilo na Roho Mtakatifu litakalopitia katika ule wakati wa Dhiki. Walio Wateule ndio watakaofaulu.

246 Ee, ningegusia kitu fulani hapa sana, kwa dakika moja hivi. Je, mwaweza kunipa dakika tatu zaidi? Je, watu wawalionyakuliwa waitwaje, masalio? Sivyo? Vema...Ni—ninakusudia Bi—Bibi—arusi. Sasa, masalio waliachwa.

247 Naam, mwanamke aendapo kukata bombwe la rinda, nena kuhusu hiyo. Yeye atandika jora (sivyo?), kile kipande cha jora. Naye hutandaza bombwe lake. Naye anachora sehemu hilo bombwe litakayokatiwa. Sivyo?

248 Ewe ndugu, hili hakika lakufurahisha! Nani anayechagua? Mungu hufanya uchaguzi! Sivyo? Si mimi nisema, ni Yeye aseme. Na Yeye huweka bombe juu ta yule Yeye amtakaye. Sivyo?

249 Sasa, kulikuweko wanawali kumi waliokwenda kumlaki Bwana arusi. Sivyo?

250 Uanawali ni nini? *Uanawali* maana yake “safi, takatifu.” Sivyo? Msichana mwanamwali ni nani? Ni msichana ambaye hajaguswa, yeye ni bikira. Nini kilicho kisafi, kama halzeti safi? Yamaanisha imefanywa kuwa mvuke na kuugeuza kuwa mafuta tena mpaka yako katika uwanawali wake, ni masafi. Dhahabu safi ni nini? Ni wakati taka zote...imepitishwa kwa moto na kila kitu na kuchemshwa na kuondoa taka zote. Sivyo? Vyuma vyote na mrututu, na na kadhalika, vimeyeyushwa na kuondolewa, iko tu katika uanawali wake.

251 Sasa, hao kumi walikwenda kumlaki Bwana-arusi. Yesu alisema hivyo. Sivyo? Wangapi wanakubaliana na hilo, semeni “Amina.” [Kusanyiko lasema, “Amina!”—Mh.] Kumi walienda kumlaki. Sasa, tazama, hao wote walikuwa watakatifu. Vema, kuwa *watakatifu* iliwapasa “kutakaswa,” kwa sababu huko ndiko kusafishwa pekee, kijito kitakatifu alichu nacho Mungu, ni utakaso. Sivyo?

252 Sasa, tazama. Wao wote kumi walikuwa wametakaswa, bali watano hawakuwa na mafuta yo yote katika taa zao, na watano walikuwa na Mafuta katika taa zao. Sivyo? *Mafuta* yanaainisha nini? Sasa, si usafi, uanawali. *Mafuta* yaainisha “Roho Mtakatifu.”

253 Sasa, nikisema hili ku...na kuudhi kidogo, sikusudii jinsi nifanyavyo. Sasa, mniwie radhi, na msikose kuja kanisani. Mimi nimo mimbarani humu kujaribu kuwasaidia. Ona? Sasa, tazama, hebu niwaonyesheni.

254 Hakuna kanisa duniani ambalo lingeshi kisafi kuliko Wanazarini katika mafundisho yao, Pilgrim Holiness na mengineyo. Sivo? Wao wanaamini kabisa katika usafi wa kutakaswa, si...hata juu ya wanawake wao kuvaa pete, na kadhalika. Usafi na utakaso, kwa kila njia, wanaviamini. Dhehebu la Holiness, wote washikilia torati, hayo ndiyo mafundisho yao, wanayaamini. Utakatifu! Wanawake huwa na nywele ndefu na rinda refu. Wanaume hata hawapaswi kukunja mikono ya shati zao, wengi wao. Kila kitu, si hata kugusa... kuvuta sigara, kunywa pombe, lo lote...Hakuna yo yote ya hayo, ona. Utakatifu! Hungeishi msafi zaidi.

255 Lakini kanisa lilo hilo la Nazarini, kama mtu angenena kwa lugha kanisani, angefukuzwa nje. Nao walisema, hata hawangeketi pamoja na mmoja wao. Sasa, hilo ni kweli. Kama huliadini, jaribu mara moja, lichunguze. Lichunguze wakati mmoja. Wanachukia hata wazo lake. Wao walisema, “Ni lbilisi!”

256 Watano wao...Kumi wao walikuwa wanawali. Watano walikuwa werevu hao waliokuwa na Mafuta katika taa zao, na hao wengine watano walikuwa wasafi na watakatifu vivyo hivyo lakini wao hawakuwa na Mafuta (walikuwa wametakaswa, hawakuwa na Roho Mtakatifu).

257 “Kwa maana wako watatu washuhudiaio duniani; maji, damu, Roho.” Yohana Mt. 5:7, samahani. 1 Yohana 5:7 kasema “Wako watatu washuhudiaio Mbinguni; Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, hawa watatu ni Mmoja. Kisha wako watatu washuhudiaio duniani: maji, damu na Roho, si moja bali hupatana kwa habari moja.”

258 Sasa, huwezi kuwa na Baba bila kuwa na Mwana. Huwezi kuwa na Roho Mtakatifu bila kuwa na Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Wao ni mmoja. Wewe...Hawatengani.

259 Lakini waweza kuhesabiwa haki bila kutakaswa. Na waweza kutakaswa bila kuwa na Roho Mtakatifu; uwe msafi, uishi maisha masafi, na uwe na aina ya utauwa, na ukane Nguvu za uponyaji na kunena kwa lugha na zile karama kuu za Mungu (na kila moja wazo ndani Mle).

260 Ndio hao wale wanawali watano wenye busara waliokuwa na Mafuta taani mwao, Imani ya kunyakuliwa, wakiadini ishara zote, maajabu, nabii, na kila kitu. Na hawa watano waliokatwa kwa wale masalio wakanyakuliwa.

261 Na wengine wao wangali wanawali na hawatapotea, bali watapitia katika ule wakati wa Dhiki. Yesu alisema “Kutakuwa...”

262 Nao walisema—walisema, “Tupeni Mafuta yenu kidogo, tunataka Roho Mtakatifu sasa.”

263 Sasa, ye yote ajua Roho Mtakatifu, Zekaria 4, na, eh, Yakobo 5:14, nyote mwajua kuwa—kuwa hayo yawakilisha Roho Mtakatifu. Sasa, wao walisema . . . Hiyo ndiyo sababu sisi hupaka mafuta, kuwakilisha Roho Mtakatifu; sasa, “Mafuta ya Roho,” Biblia ilisema.

264 Sasa, hawa walikuwa na Roho Mtakatifu; na hawa walikuwa wametakaswa. Hawa walikuwa wametakaswa pamoja na Roho Mtakatifu, wakiadini matukio yote na kila kitu cha Nguvu za Mungu. Kila kitu Mungu alichonena hapa, wao walikuwa nacho, wakikiamini. Hawa walinyakuliwa.

265 Nao hawa wakasema, “Tupeni, sisi, sasa.”

266 Kasema, “Tunayo tu ya kututosha kutuingiza,” nao wakatwaliwa kwa Kunyakuliwa.

267 Na ilisema, “Shikeni njia mwende kwa wauzao mkajinunulie kidogo.” Yesu alisema. Nao walienda kujaribu kuomba wapate wakati huo, wampokee Roho Mtakatifu, bali wakati wa Mataifa ulikuwa umekwisha na mateso yakaanza. Naye alisema, “Walitupwa nje gizani ambapo kulikuwa na kulia na kuomboleza na kusaga meno.” Lakini katika ufufuo wa pili watakuwa wale kondoo watakaobaguliwa pamoja na wale mbuzi, bali si Bibi-arusi kamwe, si Wateule kamwe. Hao ndio masalio ya yule Mzao wa mwanamke.

268 Masalio ni nini? Sehemu iliyokatwa, iliyoachwa. Aina ile ile ya bidhaa. Sivyo? Unaenda kukata rinda lako la bafta, nawe unakitandaza kile kitambaa kikubwa cha bafta na kukikata. Ni juu yako mahali uwekapo bombwe lako. Ni juu ya Mungu mahali anapoweka hiyo bombwe, Yeye huikata. Sivyo? Na sasa hii, bafta ile nyingine iliyobaki hapa, ni bafta, ni nzuri tu kama iliyo kwenye rinda lile. Sivyo? Lakini ni uchaguzi wa Mungu. Mungu huchagua Kanisa Lake, Mungu huchagua asili Kanisa Lake; Mungu alichagua hapa, alichagua awali Kanisa Lake, naye analichukua Kanisa hilo! Na mabaki yanaachwa yapitie katika wakati wa ile Dhiki.

269 Na hapo ndipo wanavyuoni wengi na Biblia siku hizi hutatanishwa, wakidhani kwamba Bibi-arusi yuko kule katika ile Dhiki. Mtu fulani aliniambia, kasema, “Singekuambia wewe, Ndugu Branham.” Kasema, “Nilimwona Bibi-arusi Mbinguni. Na joka kubwa jekundu likimwaga maji toka kinywani mwake lifanye vita na Bibi-arusi. Na wale mia na arobaini na nne elfu, ambao ni Bibi-arusi, wamesimama kwenye mlima Sinai.”

270 Nilisema, “Ee, la. La. La. Umeifarakanisha yote. Bibi-arusi alikuwa Mbinguni.” Na *masalio* ya ule Uzao wa mwanamke, si yeye. . . si lile bombwe masalio yalikuwa pale, na yale mateso (Milki ya Rumi) wakati Ukatoliki utakapimarishwa

nao wataungana na kuunganisha mamlaka yao pamoja na lile kanisa Kuu.

271 Naam, walikuwa nayo papo... Yalikuwa kwenye televisheni usiku uliopita. Kanisa la Methodist linajaribu kuunganisha Methodist na Batisti na makanisa yote ya Kristo yanajaribu kuungana na Ukatoliki na kusimama mbele ya madhabahu moja wazi. Askofu yule alisemaje alipohojiwa usiku uliopita, kuhusu Komunisti pale? Nilikuwa nimesimama nikitazama televisheni mimi mwenyewe. Makundi yao yote! Na wakati huo utimiapo, kutazuka mateso na Roho Mtakatifu atawashukia Wamethodisti na Wabatisti. Nao wote watanena kwa lugha, watamsifu Mungu na kuponya wangojwa na kutabiri, na ishara zote na maaajabu yatakuwa yakitendeka. Wateule watanyakuliwa, na wale waliosalia wataachwa hapa wapitie katika wakati wa ile Dhiki. Na mwishoni mwa wakati huo, watakapoona yale yametendeka, itawalazimu kufia imani yao.

272 Ndipo tazama, mwasema, "Vema, sasa, Ndugu Branham, wakusudia kuniambia kutakuwako na... kuwa—kuwa watu hao ndio watakaokuwa kwenye ile Hukumu ya Kiti Cheupe cha Enzi?" Wata... Bibi-arusi hatahukumiwa. La, bwana. Yeye yuko ndani ya Kristo, unaingiaje katika Kristo? "Kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa katika Mwili mmoja." Sivyo?

273 Sasa, tazama hapa. Biblia ilisema, "Hukumu ikawekwa, na Vitabu vikafunuliwa." Sivyo? Vitabu vya wenye dhambi. "Na Kitabu kingine kilifunguliwa," ambacho ni kile Kitabu cha Uzima, na kila mtu alihukumiwa hivyo. Sivyo? Na nani aliyekuwa akihukumu? Yesu na watakatifu. Yeye alisema, "Yeye alikuja na kumtumikia yule Mzee wa Zamani ambaye nywele Zake zilikuwa kama sufu." Na kasema, "Makumi elfu mara kumi elfu walikuja pamoja Naye, na kumtumikia katika Hukumu ile." Hapa Yesu arudi kama Mfalme na Malkia, Arusi imekwisha, na Yeye amekwishaoa. Mfalme na Malkia wamesimama hapa. Na pale lasimama lile kundi la waliotakaswa, Mungu alisema, "Simameni upande wangu wa kuume hapa." Hapo ndipo kile Kitabu kilipofunguliwa, walimokuwa wenye dhambi, "Nendeni upande wangu wa kushoto." Hao ndio wale ambao majina yao yaliandikwa katika kile Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo.

274 Mwasema, "Ndugu Branham, jina langu limeandikwa kule, nitaenda!" Ngoja kidogo! Yuda Iskariote alikuwa ametakaswa, whiu! Ndugu, amka sasa, tafadhali, ili upate Hili, uone.

275 Yuda Iskariote, roho yake ndiyo mpinga-Kristo siku hizi. Mwajua hilo. Yesu alikuwa Mwana wa Mungu, alitoka kwa Mungu na alirudi kwa Mungu; Yuda alikuwa mwana wa upotevu, alitoka kuzimuni na akarudi kuzimuni. Yesu alimchukua mwenye dhambi aliyetubu akaenda Naye; Yuda akamchukua yule asiyetubu akaenda naye, "Kama wewe ni! Kama! Kama! Kama wewe u mponyaji wa Kiungu, fanya *hili*. Kama wewe ni

Hiki, fanya hili. (Ona, hiyo alama ya maswali kote kwenye Neno la Mungu.) “Siku za miujiza zimekwisha. Kama ndivyo ilivyo, nionyeshe *hili*. Kama! Kama! Kama!” Ona?

“Lote ni kweli,” Mungu alisema.

276 Sasa tazama. Yuda Iskariote alitakaswa kwa imani, na alimwamini Bwana Yesu Kristo na akabatizwa. Biblia ilisema, “Yesu—Yesu aliwabatiza wanafunzi, wanafunzi Wake.” Vema.

277 Yohana Mt. 17:17, kabla hajawatuma woa, Yeye alisema, “Uwatakase, Baba, kwa ile Kweli; Neno Lako ndiyo Kweli.” Naye alikuwa ndiye hilo Neno, hata kabla huo utakaso kufanywa. Yaani, “Mfano wa mbeleni, Baba, kwa Damu Yangu itakayomwagika, nawatakasa hawa.”

278 Yeye aliwapa hao uweza juu ya pepo wachafu, nao waliondoka na kuwatoa pepo. Sivyo? Nao wakaponya wagonjwa. Sivyo? Nao walirudi, wametakaswa, wakifurahi, wakirukaruka, wakipiga shangwe, na kumtukuza Mungu. Sivyo? Na kasema, “Hata pepo wanatutii sisi.”

279 Na Yesu kasema, “Msifurahi kwa sababu pepo wanawatiini ninyi, bali furahini kwa sababu majina yenu yameandikwa katika kile Kitabu cha Mbinguni.” Sivyo? Na Yuda Iskariote alikuwa pamoja nao, mmoja wao, aliyeitwa, akatakaswa, na jina lake likaandikwa katika kile Kitabu cha Mwana-Kondoo cha Uzima. Someni Mathayo 10 na mwone kama hilo si sahihi. Yeye aliwatuma, akawapa mamlaka juu ya pepo wachafu.

280 Sasa tazama! Vaa fulana yako ya kustahimili mshituo. Lakini Yuda alipokuja kupitia kwa kanisa lile pale, kama mweka hazina wa kanisa, akifanya kazi na mchungaji wake, yule yule. . . Yesu. Lakini wakati wa Pentekoste ulipotimia, yeye akadhihirika. Yeye alionyesha alivyokuwa. Na akiwa—akiwa mheshimiwa kutosha, alijiangamiza mwenyewe na kujiangika mkuyuni, kutimiza unabii. Na roho huyo wa Yuda atajitokeza tena na kumwamini Bwana Yesu Kristo. Kama Yesu alivyosema, “Mashetani wanaamini na kutetemeka.” Yeye atakuja hadi hapa na kufundisha utakaso, maisha masafi na matakatifu iwezekanavyo; lakini inapofikia ubatizo wa Roho Mtakatifu na karama za Roho, yeye atavikana! Yeye atonekana wazi kila wakati. Roho yule ndiye huyo.

281 Tazama! Naye alisema, “Jihadhari!” Mathayo 24, tena. “Roho hizo mbili zitafanana sana hata zingeweza kuwateza wa lio Wateule. . .” Sivyo? Ambapo mfano ule ume—umewekwa. . . Ndugu, heri uamini wahubiri wa mtindo wa kale, waliojazwa Roho Mtakatifu humu na ukubalike kwa Mungu. Msiwe na mfano wa utauwa na kukana Nguvu zake. Amina! Kila mtu ajisikia vizuri? [Kusanyiko lasema, “Amina!”—Mh.]

Sisi sote tutakapofika Mbinguni,
Itakuwa siku ya furaha namna gani!
Sote tutakapomwona Yesu,
Tutaimba na kushangilia huo ushindi.

Sisi sote tutakapofika Mbinguni,
Itakuwa siku ya furaha namna gani!
Sote tutakapomwona Yesu.
Tutaimba na kushangilia ushindi.

²⁸² Haleluya! Hebu tusimame kwa muda mfupi tu. Wangapi wanampenda kwa moyo wenu wote? Inua mkono wako, useme, “Bwana asifiwe!” [Kusanyiko lasema, “Bwana asifiwe!”—Mh.] “Bwana, ninaamini Injili yote.” [Kusanyio lasema, “Bwana, ninaamini Injili yote.”—Mh.] “Nisaidie kuwa mtumishi Wako.” [Kusanyiko lasema, “Nisaidie kuwa mtumishi Wako.”—Mh.] Haleluya! Haleluya! Je, mwampenda? [Kusanyiko lasema, “Amina!”—Mh.] Katika Biblia wao. . .

²⁸³ Mwanamke fulani aliniambia siku moja . . . mvulana, huenda yeye anasikiza usiku huu, yeye anaishi tu ng’ambo ya njia hii ya mji. Yeye alikuja pale. Na Dada Lula aliyekuwa akija hapa kanisani, alikuwa akipiga shangwe nyuma kule. Nilikuwa nahubiri, Ndugu Neville. Na mvulana yule akaniambia. . . Naam, yeye alikuwa mwalimu wa shule ya Jumapili chini hapa kwa kanisa la First Baptist. Yeye alisema, “Billy, nilikuwa nafurahia mahubiri yako hadi mwanamke yule alipoanza kulia na kupayuka-payuka, “Asante Ewe, Yesu! Bwana asifiwe!” Mara kwa mara” kasema, “mtu fulani akasema,” (Ndugu Seward) “alipayuka, ‘Bwana asifiwe! Amina!’” Nami nilikuwa nikihubiri juu ya *Kupoteza Haki Yako ya Mzaliwa wa Kwanza*, Esau aliuza Haki yake ya Mzaliwa wa Kwanza. Nami nilikuwa nikiendelea, nao walikuwa tu wakipiga ma—makelele, wakiendelea. Kasema, “Ooooho,” kasema, “hilo—hilo lanifanya nisikie baridi mgongoni.” Kasema, “Singestahimili hilo!”

²⁸⁴ Nilisema “Ndugu, kama ungalienda Mbinguni ungalikufa kwa baridi.” Nilisema, “Bila shaka kuna shangwe Mbinguni, mchana na usiku.” Ndivyo ilivyo, ndugu. Ee, naam, bwana!

Ee, nataka kumwona, kuutazama uso Wake,
Nikaimbe Milele juu ya neema Yake iokoayo.
Kwenye njia za mji wa Utukufuni nikapaze
sauti yangu;
Masumbuko yote yamekwisha, hatimaye niko
nyumbani, raha daima.

Ee, nataka kumwona, kuutazama uso Wake.
Huko niishi milele kwa ajili ya neema Yake
iokoaye;

Kwenye njia za Utukufuni nikapaze sauti
yangu;
Masumbuko yote yamekwisha, hatimaye niko
nyumbani, raha mustarehe.

²⁸⁵ Amina! Vema, Ndugu Neville. Mungu akubariki. Nenda pale
juu kafunge.



Mwenendo, Utaratibu Mafundisho ya Kanisa, Kitabu Cha Kwanza
(Conduct, Order And Doctrine Of The Church, Volume One)

Jumbe hiza za Ndugu William Marrion Branham, ziliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali zilitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings. Ilichapishwa tena katika mwaka wa 2013.

SWAHILI

©2009 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org